JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO

CHUMBA CHA WATEULE

# PENDEKEZO LA KATIBA

## YA
## JAMHURI YA KIDEMOKRASIA
## YA KONGO

KINSHASA, MAY 2005

**TAFSIRI YA KISWAHILI YA**
**AWAZI NENGO Meme**
KIKUNDI CHA  YA MGAMBO

# MADHUMUNI YA KAZI HII

Tangu kujinyakulia uhuru wake tarehe 30 yuni 1960, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inakabiliwa na misukosuko ya kisiasa isiyomalizika ambayo moja katika visa muhimu vinayoisababisha ni mapingano kuhusu uhalali wa vyumba vya utawala na watawala wenyewe.

Kwa kusudi ya kutokomeza kabisa mapingano haya ya uhalali wa utawala na kuipa taifa bahati ya kujijenga vipya, wajumbe wa wafanya siasa na hao wa viongozi wa mashirika ya kijamii, wote wanaojenga mihimili ya taifa, wamekutana kunako mjadala kati ya wakongomani na kuafikiana kwa hicho tunachokiita leo **Makubaliano ya jumla na ya jumuiya**, iliyotiwa saini mjini Pretoria huko Afrika ya kusini tarehe 17 desemba 2002, ili ipandwe nchini majira mapya ya kisiasa kwa msingi wa katiba mpya ya kidemokrasia ambayo itawapa nafasi raia wakongomani kujichagulia bila bughuza yoyote viongozi wao kwa kupitia machaguzi huru, ya wazi na ya kuaminika, kwa mfumo wa vyama vingi.

Ni katika juhudi ya kudhihirisha manuwizi hayo ya wajumbe kunako mjadala wa wakongomani, ndio Chumba cha wazee ama SENETI, kilichoundwa kwa mujibu wa makubaliano ya jumla, kilipeleka mbele ya Chumba cha Wateule, kufwatana na maagizo ya kifungo cha 104 cha Katiba ya mpito, muswada wa kwanza wa katiba mpya ambao umejadiliwa na kuwafikiwa na Chumba hicho cha wateule na kuwa leo pendekezo la katiba la kupeleka mbele ya kura ya maoni kwa kuiziniwa na raia.

Pendekezo hii ya katiba iliyowafikiwa ina fikara mazubuti zifwatazo :

## 1. KUHUSU NCHI NA ENZI ZAKE

Kwa nia, kwanza, ya kuimarisha muungano wa taifa ambao, kwa hakika, umekabiliwa na mtihani mkubwa kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivodumu kiasi na, pili, ya kuweka vituo vya chochezi ya maendeleo huko kwenyi maeneo ya msingi, mtunga katiba amefikiri vema kuigawa nchi ya Kongo katika majimbo 25 pamoja na mji wa Kinshasa, kila ile ikiwa na nafsi yake ya pekee mbele ya sharia, na kuidai iwe pembeni kabisa ya raia katika kuendesha mamlaka inayobainishwa ndani ya katiba hii.

Badala ya nyuwezo hizo, majimbo yanapewa mamlaka mengine ambayo yanayaendesha kwa kusharikiana na Serikali Kuu na kugawa mapato yanayopatikana kwa kiwango cha asili mia arubaini (40 %) kwa faida ya jimbo na asili mia sitini (60 %) kwa faida ya serikali kuu.

Ikitokea hitilafu yoyote kati ya serikali kuu na majimbo kuhusu kulimiliki jambo fulani, Korti Kuu ya Katiba ndio chumba pekee kinachopewa uwezo wa kuamua.

Majimbo yanatawaliwa na serikali ya jimbo pamoja na bunge la jimbo na kila ile inagawanyika kwa maeneo inayojimiliki ambayo ni mitaa, wilaya, matarafa na maeneo ya usultani wa asili.

Tena, katiba hii inazidi kusisitiza fundisho muhimu ya demokrasia isemayo kwamba wazifa wote, utawala wote, unatoka kwa umma ambao ndio mwenye enzi wa kwanza.

Umma huo unaizihirisha matakwa yake katika mfumo wa vyama vingi, mfumo ambao unatiliwa mkazo na katiba na kuifanya kuwa hatia ya usaliti jaribio ya kurudisha tena nchini chama cha pekee.

Ama kuhusu uraia, mtunga katiba anabaki imara na kuupwekesha uraia wa Kongo ambao hauruhusiwe kuchanganywa na uraia wa nchi nyingine yoyote.

## 2. KUHUSU HAKI ZA MWANAADAMU, HURU ZA MSINGI NA MAPASHWA YA WANANCHI NA YA SERIKALI

Mtunga katiba anapendelea kuhakikisha msimamo wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo wa kutetea na kulingania haki za mwanaadamu na huru za msingi kama zinavyobainishwa na vyombo vya sharia vya kimataifa.
Ni hivi basi, haki na huru hizo zinatiwa miongoni mwa vifungo muhimu kabisa vya katiba.

Na zaidi ya hayo, kuhusiana na maendeleo ya ulimwengu wa leo, katiba hii inaupa nafasi kubwa kabisa na kuutilia mkazo mfumo wa usawa kati ya wanaume na wanawake.

## 3. KUHUSU MPANGO WA KUENDESHA UTAWALA

Kwa mujibu wa katiba hii, vyumba vya kuendesha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni vifwatavyo :

- Rais wa Jamhuri
- Bunge
- Serikali
- Korti na Mahakama.

Shabaha hasa iliyoko katika kuvipanga vyumba kama hivyo ni :

1. kuzamini mwenendo wa maafikiano kati ya viungo vya utawala;
2. kuepuka mivutano kati ya watawala;
3. kuinua nchi kwa hali ya taifa ya uhaki;
4. kuzuwiya jaribio lolote la udikteta;
5. kuzamini uongozi mzuri;
6. kulaani hali ya kukosa azabu zidi ya makosa ya watawala;
7. kupanga jinsi ya kuachiana mamlaka kwa njia ya demokrasia.

Na ndio sababu, upande moja, muhula wa rais wa Jamhuri ni wa miaka mitano na uwezekano wa kurudilia mara moja tu na, upande mwengine, Rais wa Jamhuri anaendesha mamlaka yake ya mdhamini wa katiba, wa uhuru wa taifa, wa mipaka ya nchi, wa enzi ya taifa, wa mikataba na makubaliano ya kimataifa, wa muongozi na hiyo ya refa wa uendeshaji kawaida wa vyumba vya serikali, kwa mawasiliano na serikali, chini ya uchunguzi wa Bunge.

Hati zote atazosaini kuhusiana na mambo inayohusu mamlaka ya serikali ao na uwezo wa mawaziri, zitatiwa sahihi na waziri mkuu ambaye anajukumika hivi mbele ya Chumba cha wateule.

Zaidi ya hayo, siasa ya njee, ulinzi na usalama, ambavyo hapo zamani vilikuwa ni siri pekee ya Rais wa Jamhuri, leo vinakuwa vya maafikiano kati yake na serikali.

Chini ya usimamizi na uongozi wa waziri mkuu, serikali inabaki kinara cha uendeshaji wa siasa ya taifa ambayo inapangwa kwa maafikiano na Rais wa Jamhuri.

Serikali inachunguzwa na Chumba cha wateule kufwatana na matendo na uongozi wake na inaweza kuazibiwa kwa kuwafiki muswada wa lawama. Ama tena Chumba cha wateule kinaweza kuwashutumu kibinafsi memba wa serikali kwa njia ya muswada wa tuhuma.

Chumba cha wateule pamoja na seneti, vikijumuika katika kongresi, vinakuwa na uwezo wa kuwakatia mashtaka Rais wa Jamhuri na Waziri Mkuu mbele ya Korti Kuu ya Katiba kwa hatia ya usaliti ao ya kukonyezwa.

Hata wakiwa na uwezo kamili wa kutunga sharia na kuchungua serikali, wabunge hawachukuliwi na heshima ya juu ya sharia. Hifadhi yao binafsi inaweza kuvuliwa na Rais wa Jamhuri anaweza kuipiga marufuku Bunge nzima ikihitilafiana vikali na serikali.

Katiba hii inasisitiza uhuru wa mahakama ambayo memba wake wanaongozwa tu na halmashauri kuu ya uamzi inayokaliwa na mahakimu watupu.

Kwa kukuza taalima na busara katika tafakari ya mambo mbalimbali, Korti na mahakama inagawanyika kwa tabaka tatu :

1. Vituo vinavyohusika na maamzi ya hatia za kawaida chini ya uchunguzi wa mahakama kuu;
2. Vituo vinavohusika na hatia za uongozi, chini ya uchunguzi wa Halmashauri Kuu ya Serikali;
3. Korti Kuu ya Katiba.

Vifungo maalumu vya katiba vinafafanua mipaka ya uwezo wa serikali kuu na wa majimbo, na mambo yanayoweza kuendeshwa kwa masharikiano ya daraja hizo mbili za utawala.

Ama kwa kukuza maafikiano kati ya majimbo yenyewe kwa yenyewe na kati ya majimbo na serikali kuu, inaundwa Baraza ya maliwali, chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri, baraza inayopewa fursa ya kuwa mshauri wa daraja hizo mbili za utawala wa nchi.

Tena, kuhusiana na wajibu wa mfungamano kati ya vikundi mbalimbali vinavyounda taifa, inahimizwa kuundwa mfuko wa kusawazisha mapato chini ya uongozi wa serikali.

Ukitizamwa pia uwingi wa shida za maendeleo, na za kijamii zinazoikabili Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mtunga katiba anaunda halmashauri ya kiuchumi na ya kijamii na kuihusisha hivi

na kutoa fikara na maoni kwa yanayohusu maendeleo na ujamii, kuipeleka kwa Rais wa Jamhuri, mbele ya Bunge na mbele ya serikali.

Na kwa kuzidi kukuza mfumo wa demokrasia nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, katiba hii inabakisha viungo viwili vya kulingania demokrasia, navyo ni Tume Huru ya taifa kuhusu uchaguzi na halmashauri ya mitambo ya habari na mawasiliano. Ya kwanza itahusika kwa kila wakati na kupanga taratibu za uchaguzi na ya pili italingania uhuru na kinga ya mitambo ya habari na njia nyingine ya mawasiliano ya umma katika kuheshimu sharia.

## 4. KUHUSU KUREKEBISHA KATIBA

Kwa kukinga nguzo za demokrasia zilizomo katika katiba hii zidi ya kasoro na mishkili ya kisiasa na majaribio ya mabadiliko ya zarura, mipango kuhusu umbo la kijamhuri, mfumo wa kura ya umma, serikali ya uwakilishaji wa taifa nzima, idadi ya awamu za Rais wa Jamhuri, uhuru wa mahakama, mfumo wa vyama vya siasa na mashirika ya utetezi wa wafanya kazi, haiwezi kamwe kubadilishwa ao kurekebishwa.

X X

X

Tizama mistari mikubwa inayoijenga katiba hii.

Chumba cha Seneti kimependekeza;

Chumba cha wateule kimewafiki;

Raia wakongomani wamekubalisha
Kwa kura ya maoni iliyofanyika tarehe...... hadi ........

Rais wa Jamhuri anaizinisha Katiba ifwatayo.

## KIINGILIO

SISI, RAIA WAKONGOMANI
Tukishikamana kwa kadara na kwa historia katika mfumo wa uhuru, undugu, mfungamano, uhaki, amani na kazi;

Kwa utashi tunao wa kuijenga kati ya Afrika nchi ya haki, taifa la nguvu na la ustawi, kwa misingi ya demokrasia ya kweli katika shuruli za kisiasa, za kiuchumi, za kijamii na za kitamaduni;

Tukikiri kwamba zulma na vinyume vyake, kukosekana azabu zidi ya makosa mbalimbali, mapendelevu ya familia, ya kabila, ya kikao, ya jimbo na mengine ya kuvifanana ndio, kufwatana na matokeo yao mabaya, vimesababisha kuchafuka kwa mila mizuri na kuisindikiza nchi katika udidimizi wa mwisho;

Tukihakikisha hapa makusudio yetu ya kulingania na kuimarisha uhuru, muungano wa taifa katika tofauti zetu na maumbile yetu ya ndani;

Tukisisitiza kujiunga kwa tangazo la kimataifa kuhusu haki za mwanaadamu, ratiba ya kiafrika kuhusu haki za mwanaadamu na za nyumma, mikataba ya jumuiya ya madola kuhusu haki za mtoto na

za mwanamke, hususa hiyo ya usawa kati ya mume na muke katika uwakilishi kunako vyumba vya utawala, na kwa vyombo vingine vya kimataifa kuhusu kinga na ulinganiaji wa haki za watu;

Kwa nia ya kuyachochea mataifa yote ya Afrika kujiunga pamoja na kutumika mkono kwa mkono kwa kukuza na kudumisha umoja wa kiafrika kwa kupitia mashirika ya kiafrika na hayo ya muungano wa sehemu mbalimbali za bara ili kuwafaidia raia mipango mizuri ya ukuzo na maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi;

Tukikubali makusudio ya kukuza mawasiliano ya kimataifa inayofaidia pande zote na kuyapatanisha nyumma za ulimwengu katika heshima ya hadhi ya kila umma, enzi na mipaka ya kila nchi;

Tukisisitiza haki zetu ambazo hazizulumiwe kamwe za kujiendesha kwa ihtiari na kuendeleza majira yetu ya kisiasa, ya kiuchumi, ya kijamii na ya kitamaduni, kwa taalima zetu wenyewe;

Tukizibiti jukumu zetu mbele ya Mweny’Enzi Mungu, mbele ya taifa, mbele ya Afrika na mbele ya ulimwengu mzima;

Tunakiri leo na kutangaza wazi kwamba tunaikubali katiba hii.

# MLANGO WA KWANZA

## MIPANGO YA AWALI

# KIPINDI CHA KWANZA

## NCHI NA ENZI ZAKE

### SEHEMU YA KWANZA : KUHUSU NCHI

#### Kifungo cha 1*a*

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, katika mipaka yake ya tarehe 30 yuni 1960, ni nchi ya haki, huru, yenyi enzi, ya muungano na isiyogawanyika, ya ujamii, inayoendeshwa kwa mfumo wa demokrasia na isiyotegemea dini yoyote.

Kitambulisho chake ni bendera ya rangi ya samawi ikichapwa nyota ya rangi ya manjano kwenyi pembe la juu kushoto, ikikatizwa kati kwa kati kuanzia pembe la chini kushoto hadi pembe la juu kuume kwa ukanda mwekundu unaozingwa pande zote na vistari vidogo vya rangi ya manjano.

Sifa zake kuu ni Uhaki – Amani – Kazi.

Nishani yake inaundwa na kichwa cha chui kikizingwa upande moja na pembe ya tembo na upande mwengine na mkuki, vyote vikiikazwa juu ya jiwe;

Wimbo wa taifa huitwa “simameni wima, wakongomani”
Pesa zake huitwa Franka za Kongo.

Lugha yake rasmi ya matumizi ni kifaransa.
Lugha zake za taifa ni kikongo, Kiswahili, Lingala na Tshiluba. Serikali inashurulikia ukuzaji wa lugha hizo bila ubaguzi wowote.

Lugha zingine za kyenyeji ni miongoni mwa rasilimali ya kitamaduni ya Kongo ambayo inakingwa na serikali.

Kifungo cha 2*/*

Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo inaundwa na Mji wa Kinshasa na majimbo ishirini na tano (25) kila ile ikiwa na nafsi yake mbele ya sharia.

Nayo majimbo ni: (1)Ekwatori, (2)Ituri, (3)Kasai, (4) Kasai ya mashariki, (5)Katanga ya juu, (6)Kivu ya kaskazini, (7)Kivu ya kusini, (8)Kongo ya kati, (9)Kwango, (10)Kwilu (11)Lomami, (12)Lomami ya juu, (13)Lualaba, (14)Lulua, (15)Mai Ndombe,

(16)Maniema, (17)Mongala, (18)Sankuru (19)Tanganyika, (20)Tshopo, (21)Tshuapa, (22)Ubangi ya kaskazini, (23)Ubangi ya kusini, (24)Uele ya chini, (25)Uele ya juu.

Kinshasa ndio mji mkuu wa Jamhuri na makao ya vyumba vya serikali kuu.

Mji wa Kinshasa una daraja ya jimbo.

Hauwezi kuhamishwa mji mkuu ila kwa kupitia kura ya maoni ya raia.

Mgao wa mamlaka kati ya serikali kuu na majimbo unafanyika kuhusiana na mipango ya mlango wa nne wa Katiba hii.

Mipaka ya majimbo, kama vile hiyo ya mji wa Kinshasa, inabainishwa na sharia maalumu ya uongozi.

Kifungo cha 3*u*

Majimbo na maeneo inayojimiliki katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inayo, kila ile nafsi yake mbele ya sharia, na inaongozwa na viungo vya kyenyeji.
Nayo maeneo inayojimiliki ni Mitaa, mawilaya, matarafa na maeneo ya usultani wa asili.

Maeneo haya yanapewa uhuru kamili wa kujiendesha na hasa uwezo wa matumizi ya rasilimami yao ya kiuchumi, ya kiufundi, ya kimali na ya watu.

Mpango, mipangilio na uendeshaji wa maeneo inayojimiliki, kama vile namna ya mawasiliano yake na serikali kuu pia na majimbo, vinabainishwa na sharia maalumu.

Kifungo cha 4*e*

Majimbo mengine mapya na maeneo mengine ya kujimiliki yanaweza kuundwa kwa kuchanganya ao kwa kuachanisha hiyo iliyoko katika kutekeleza masharti inayopangwa na katiba na taratibu inayobainishwa na sharia.

## SEHEMU YA PILI : KUHUSU ENZI

Kifungo cha 5*o*

Enzi ya taifa inamilikiwa na umma. Wazifa wote umo mikononi mwa umma ambao unauendesha moja kwa moja kwa njia ya kura ya maoni ao ya uchaguzi, ama tena kwa niaba ya mawakili wake.

Halina nafasi kundi lolote la watu, ama mtu yeyote binafsi, kujivika peke yake enzi ya umma.

Sharia maalumu inabainisha mipango ya kufanya uchaguzi na kura ya maoni.

Kura inawahusu raia wote, katika usawa na huwa siri binafsi. Kura inaweza kuwa ya moja kwa moja au kwa njia ya mawakili.

Bila kuhasiri mipango ya vifungo vya 72, 102 na 106 vya katiba hii, wana haki ya kupiga kura na ya kuwania kura kwa mujibu wa sharia, wakongomani wote, wa kike kama vile wa kiume, wenyi umri wa miaka kumi na minane (18) timamu, na wenye kuwa na haki zao kamili za uraia na za kisiasa.

## Kifungo cha 6*a*

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inajuzisha mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mkongomani yeyote anayekamilikiwa haki zake za uraia na za kisiasa ana haki ya kuunda chama na hiari ya kujiunga kunako chama anachokitaka.

Vyama vya siasa vinasaidia raia kutoa maoni yao kwa njia ya kura, kukuza fahamu na zamiri ya raia na kuwajuvya vilivyo elimu ya uraia.

Vyama vinaachiwa nafasi ya kuundwa na kuendesha shuruli zao bila tatizo lolote, katika kuheshimu sharia, mipango ya usalama na mila mizuri.

Vyama vya siasa vinalazimika kuheshimu misingi ya demokrasia ya uwingi, muungano na enzi za taifa.

Vyama vya siasa vinaweza kupokea kutoka kwa serikali misaada ya mali kwa kuendesha kampeni za uchaguzi na shuruli zao zingine, kwa masharti inayopangwa na sharia.

Kifungo cha 7*a*

Hawezi kabisa mtu yeyote, kwa hali yoyote ile na kwa sababu yoyote ile, kurudisha tena nchini ama katika sehemu fulani ya nchi, mfumo wa chama cha pekee.

Kurudisha tena chama cha pekee nchini kunahusiana na hatia ya usaliti isiyokuwa na mda kwa kuazibiwa na sharia.

Kifungo cha 8*e*

Unahalalishwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo upinzani wa kisiasa.

Haki kuhusiana na kuundwa kwake, shuruli zake na kugombea kwake utawala kwa njia halali ya kidemokrasia,

zinatukuka, wala hazina mipaka ila hiyo inayopangwa juu ya vyama vya siasa na shuruli zingine za kisiasa kwa mujibu wa katiba na kwa mpango wa sharia.

Sharia maalumu ya uongozi inabainisha hali ya kuwa ya upinzani wa kisiasa.

Kifungo cha 9*a*

Serikali inamiliki daima ardhi na vilivyo chini ya ardhi, mito na misitu, anga na sehemu ya jito, ya visiwa na ya bahari ya mipakani, pia na mabahari, nyika na milima iliyomo ndani ya eneo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mipango ya kumiliki na kukodisha visehemu vya mojawapo miongoni mwa rasilimali zinazotajwa hapa juu, inafafanuliwa na sharia.

## KIPINDI CHA PILI
## KUHUSU URAIA

Kifungo cha 10*i*

Uraia wa Kongo ni mmoja tu na wa pekee. Uraia wa Kongo hauchanganywe na huo wa nchi nyingine yoyote.

Uraia wa Kongo huwa wa asilia ama wa kutunukiwa binafsi.

Mkongomani wa asilia ni mtu yeyote mwenye asili yake katika makundi ya makabila ambayo watu na ardhi ndio vimeunda sehemu ya ardhi iliyopewe jina la Kongo siku ya uhuru (na kuitwa leo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo).
Sharia maalumu inafafanua jinsi ya utambuzi, kupewa, kupoteza na kurudilia vipya uraia wa Kongo.

## MLANGO WA PILI
## HAKI ZA MWANAADAMU – HURU ZA MSINGI
## MAPASHWA YA MWANANCHI NA YA SERIKALI

### KIPINDI CHA KWANZA
### HAKI ZA KIRAIA NA ZA KISIASA

#### Kifungo cha 11*a*

Wanaadamu wote wanazaliwa huru wakilingana sawa kwa hadhi na kwa haki.

Bali, haki za kisiasa ni fazila wanayopewa wakongomani peke yao, isipokuwa kwa mpango unaobainishwa na sharia maalumu.

Kifungo cha 12*i*

Wakongomani wote wanalingana sawa kwa sawa kisharia na wana haki sawasawa ya kukingwa na sharia.

Kifungo cha 13*u*

Hawezi kubaguliwa mkongomani yeyote kuhusu maadibisho ao kazi kunako taasisi za serikali ama kuhusu jambo lingine lolote, kwa mujibu wa sharia ao kwa hatua yoyote ya wakuu viongozi, ajili ya dini yake, ya asili yake, ya familia yake, ya hali yake ya maisha, ya makao yake, ya msimamo wake kisiasa, ya rangi yake, ya kabila lake, ya asili yake miongoni mwa makundi ya wachache wazalili, ya kitamaduni ama ya lugha yake.

Kifungo cha 14*e*

Viongozi watawala wanajitahidi kutokomeza hali yoyote ya ubaguzi zidi ya mwanamke na kuzamini ukingo na ukuzaji wa haki zake.

Wanahusisishwa kwa pande zote, kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, kuchukua hatua zinazostahili kwa kukuza na kuimarisha mchango wa akina mama katika mikakati yote ya maendeleo ya taifa.

Wanachukua pia hatua zinazostahili kwa kutokomeza hali yote ya ugaidi zidi ya mwanamke, iwe kwa maisha ya zahiri ao ya kipekee.

Mwanamke ana haki ya uwakilishi wa sawa kwa sawa kunako vyumba vya utawala wa taifa, wa majimbo na wa mitaa.

Serikali inazamini kuweko usawa kamili kati ya wanaume na wanawake kunako vyumba hivyo.

Sharia inabainisha jinsi ya kufaulu na haki hizo.

Kifungo cha 15*o*

Viongozi watawala wanahusika na kutokomeza ubakaji unaotumiwa kama silaha ya kuzoufisha ao ya kuvunja familia.
Bila kuhasiri mikataba na mapatano ya kimataifa, kutumia njia ya kubaka zidi ya mtu yeyote kwa lengo la kuzoufisha ama kuachanisha unyumba, ya kuteketeza kundi fulani ya watu, inahusika na hatia zidi ya walimwengu inayoazibiwa na sharia.

Kifungo cha 16*a*

Nafsi ya mwanaadamu ni tukufu.

Kila mtu ana haki ya maisha, ya uzima wa mwili wake pamoja na maendeleo ya utu wake katika kuheshimu sharia, mipango ya usalama, haki za wengine na mila mizuri.

Hawezi mtu yeyote kushikiliwa katika hali ya utumwa ao kutiwa katika hali inayoifanana.

Hawezi mtu yeyote kutendewa matendo ya utesaji, ya kuhalifu utu wake ao kupunguza heshima yake.

Hawezi mtu yeyote kulazimishwa kazi ya mkazo ao ya kushurutishwa.

Kifungo cha 17*a*

Uhuru wa nafsi unazaminiwa. Uhuru huwa ndio hali ya kawaida na kifungo huwa kitenguzi.

Hawezi mtu yeyote kushtakiwa, kuziwiliwa, kufungwa ao kuhukumiwa ila kwa mujibu wa sharia na kwa mipango inayobainishwa.

Hawezi mtu yeyote kushtakiwa kwa kitendo ao kwa jambo ambalo lilikuwa si uhalifu zidi ya sharia wakati lilitendeka ao wakati anatuhumiwa.

Hawezi kuhukumiwa mtu kwa kitendo ao kwa jambo ambalo si uhalifu zidi ya sharia wakati linatendeka na wakati wa hukumu.

Hawezi kupewa mtu azabu ya kuzidi hiyo inayopangwa wakati inafanyika hatia.

Nayo azabu aliyoamuliwa mtu itakoma kwa mujibu wa sharia inayotukia baadae :

- ikiwa kama sharia hii inaifuta;
- ikiwa kama hatia iliyosababisha azabu hiyo sio tena uhalifu zidi ya sharia.

Ama ikitukia sharia inayopunguza kiwango cha azabu ya hatia hiyo, azabu aliyopewa italinganishwa na kiwango hichi cha sasa.

Hatia zinazostahili azabu ni juu yake mtu binafsi.
Hawezi mtu yeyote kushtakiwa, kuzuwiliwa, kufungwa ao kuhukumiwa kwa makosa ya mtu mwengine.

Mtu yeyote anayetuhumiwa jambo fulani anazanika kuwa bado bila kosa lolote ila pale makosa yake itabainishwa na hukumu kamili.

Kifungo cha 18*e*

Anapozuwiliwa mtu yeyote, ana haki ya kujulishwa pale kwa pale sababu za kizuwizi, kwa lugha anayoizibiti vema, na kumjuvya pale pale tuhuma anayokabiliwa nayo.
Atafahamishwa pia, pale kwa pale, haki zake zote.

Mtu anayezuwiliwa kwa mda ana haki ya kuruhusiwa papo hapo awasiliane na jamaa lake pamoja na wakili wake.

Kizuwizi chochote hakipashwe kuzidi masaa arubaini na nane (48). Pale tu utamalizika mda huo, ataachika huru mtu huyo ao atapelekwa mbele ya kituo cha mahakama.

Mfungwa yeyote, kama vile mtu yeyote anayezuwiliwa, ana haki ya kutendewa matendo ya kulinda heshima yake, maisha yake na afia yake ya mwili na ya akili.

Kifungo cha 19*a*

Hawezi mtu yeyote kukimbizwa ama kupevushwa mbele ya jaji anayepangiwa na sharia.

Mtu yeyote ana haki ya kudai jambo lake lisikilizwe kwa makini kabisa na jaji aliye na uwezo na kwa mda unaoruhusiwa.

Haki ya kujitetea inazaminiwa na kupangwa na sharia.

Mtu yeyote ana haki ya kujitetea mwenyewe ao kwa njia ya wakili anayemchagua mwenyewe, kwa kipindi chochote cha kuendesha kesi, hata kuanzia kwa uchunguzi wa afisa wa polisi.

Ni haki yake pia kusaidiwa na wakili hata mbele ya idara za usalama.

Kifungo cha 20*i*

Kesi za korti na mahakama zinafanyika hazarani, kwa uwazi, isipokuwa tu ikionekana kama muhazara unaweza kuhatarisha usalama na mila mizuri.

Kifungo cha 21*a*

Hukumu yoyote huandikwa kunako hati ya hukumu, hubainisha visa na sababu, na hutangazwa kwenyi vikao vya mahakama.

Haki ya kukata rufaa zidi ya hukumu inazaminiwa kwa wote na kuendeshwa kwa mipango ya sharia.

Kifungo cha 22*i*

Mtu yeyote ana haki ya uhuru wa fikara, wa zamiri na wa dini.

Mtu yeyote ana haki ya kuzihirisha imani yake na dini yake, peke yake ao katika kundi, kwa siri ao kwa zahiri, kwa ibada, kwa mafundisho, kwa mazehebu ao kwa hali ya utawa, pamoja na kuheshimu mipaka ya sharia, ya ukimya, mila mizuri na haki za wengine.

Sharia inabainisha jinsi ya kuendesha haki hizo.

Kifungo cha 23*u*

Mtu yeyote ana haki na uhuru wa misemwa.

Haki hii ni pamoja na uhuru wa kuzihirisha mawazo na fikara zake kwa maneno, kwa maandishi, kwa picha pamoja na kuheshimu sharia, ukimya na mila mizuri.

Kifungo cha 24*e*

Mtu yeyote ana haki ya kupelekewa habari sahihi.

Unazaminiwa uhuru wa kutangaza na kupeperusha habari kwa njia ya redio, televisheni na magazeti ao kwa mitambo mingine katika kuheshimu mipaka ya ukimya, mila mizuri na haki za wengine.

Sharia inafafanua mipango ya kutumikisha huru hizo.

Mitambo ya habari ya serikali ni idara za umma ambazo hutumiwa sawa kwa sawa na makundi yote ya kisiasa na ya kijamii.

Hali ya mitambo hiyo ya serikali inabainishwa na sharia kwa nia ya kuheshimisha uadilifu, usawa, kutopendelea na hasa mfumo wa tofauti ya fikara katika kutangaza na kupeperusha habari.

Kifungo cha 25*o*

Uhuru wa mikutano na mihazara ya ukimya na bila silaha unazaminiwa katika kuheshimu mipaka ya sharia, usalama na mila mizuri.

Kifungo cha 26*a*

Haki ya maandamano inazaminiwa.

Maandamano yoyote ya barabarani ao mihazara ya mahala pa wazi, inawalazimu wahusikao kuijulisha kwa viongozi watawala walio na uwezo.

Hawezi mtu yeyote kuitishwa kwa mkazo kwenyi maandamano bila hiari yake mwenyewe.

Sharia inafafanua jinsi ya kufaulu na haki hiyo.

Kifungo cha 27*a*

Mkongomani yeyote ana haki ya kuwatumia wakuu viongozi, kwa peke yake ao kwa pamoja na wengine, maoni yake na kupewa jibu.
Hawezi yeyote kushtakiwa na kuhukumiwa kwa hali yoyote kwa sababu tu ya kuwaandikia viongozi maoni yake.

Kifungo cha 28*e*

Hana mkazo wowote mtu kutii amri isiyokuwa halali.

Mtu yeyote ama afisa wowote wa serikali anaodokewa na mkazo wa kutii pale tu amri anayopewa inatengua haki za mwanaadamu, huru za umma na mila mizuri.

Mwenyewe anayekataa kutii ndie anahusika na kubainisha dalili za uhalifu wa amri aliyopewa.

Kifungo cha 29*a*

Makao ya mtu inahifazika. Haitembelewi ao kusachiwa ila kwa mipango ya sharia.

Kifungo cha 30*i*

Mtu yeyote anayepatikana ndani ya ardhi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ana haki ya kujitembelea kote nchini bila tatizo lolote, kuweka makao yake mahala anapopataka, kutoka na kurudi nchini kwa mipango ya sharia.

Mkongomani yeyote hawezi kufukuzwa nje ya ardhi ya Jamhuri, kusukumwa uhamishoni ao kushurutishwa kuishi njee ya makao yake ya kawaida.

Kifungo cha 31*a*

Mtu yeyote ana haki ya hifazi ya maisha yake ya kipekee, hifazi ya barua zake, ya mazungumzo yake ya simu na ya mawasiliano yake mengine ya kipekee.

Haitenguliwi haki hii ila kwa mipango ya sharia.

Kifungo cha 32*i*

Mgeni yeyote anayeishi kisharia ndani ya eneo ya Jamhuri, anafaulu kwa kinga wanayopewa watu na mali yao kwa mipango inayobainishwa na mikataba ya kimataifa na sharia mbalimbali.
Naye pia kwa upande wake anawajibishwa kuheshimu sharia na kawaida za Jamhuri.

Kifungo cha 33*u*

Haki ya ukimbizi inajuzishwa nchini Kongo.

Pamoja na kutekeleza usalama wa taifa, na kuheshimu sharia na kawaida za Jamhuri, serikali inaweza kuwapa makimbizi ndani ya ardhi ya Jamhuri, raia wa nchi nyingine wanaotatizwa ajili ya msimamo wao, ajili ya dini yao, ya rangi yao, ya kabila yao ao ya lugha yao, ama kwa juhudi zao za kulingania na kutetea demokrasia na haki za wanaaadamu na za mataifa.

Hairuhusiwi hata kidogo mtu yeyote anayepewa hifazi hii kikawaida achukue fursa ya kufanya matendo ya kuhatarisha

usalama wa nchi yake ya asili ao wa nchi nyingine yoyote kwa kutokea ndani ya ardhi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Wakimbizi hawawezi kamwe kutolewa kwa nguvu kwa wakuu viongozi wa nchi zinazowatatiza ama kurudishwa kwa mkazo ndani ya eneo ya nchi hizo.

Kwa hali yoyote, mtu yeyote hawezi kupelekwa kwa nguvu ndani ya ardhi ya nchi ambako inajulikana kama atasulubiwa ao atapewa azabu na kutendewa matendo ya utesaji, ya kupunguza hadhi yake na utu wake.

Sharia maalumu inafafanua jinsi ya kuitumikisha haki hiyo.

Kifungo cha 34*e*

Mali ya kipekee, ya kibinafsi, inatukuzika.

Serikali inazamini haki ya kila yule kumiliki kwa upekee ama kwa niaba ya jumuiya, mali aliyoipata kwa njia ya sharia ao ya desturi.

Serikali inatilia mkazo na kuvikinga vidamu vya kipekee, viwe vya wananchi ao vya wageni.

Hawezi mtu yeyote kunyanganywa mali yake ila kwa manufaa ya umma na kwa kulipiwa faini kiasi cha kulingana na samani ya mali yake, kufwatana na mipango ya sharia.

Haiwezi kutiwa mkono mali ya mtu ila kwa amri ya maafisa wa mahakama walio na uwezo.

Kifungo cha 35*o*

Serikali inazamini fikara ya kipekee kuhusu uundaji, iwe kwa wakongomani au kwa wageni.

Inatilia mkazo na kuchochea kazi za biashara ndogo ndogo za usanii na ufundi kwa raia wakongomani pamoja na kukinga na kutetea taalima na ujuzi kwa raia.

Sharia inafafanua mipango ya kufaulu kwa haki hiyo.

Kifungo cha 36*a*

Kazi ni haki na mapashwa kwa kila mkongomani.

Serikali inazamini haki ya kupewa kazi, kinga kwa wasiokuwa na kazi na malipo adili kwa mfanya kazi inayomwezesha kuishi pamoja na jamaa lake maisha ya kawaida na kumfazilisha na kinga za ujamii kwa siku za usoni, kama vile malipo ya mwisho wa kazi na msaada wa maisha yake ya ukongwe.

Hawezi mtu yeyote kuzulumiwa katika kazi yake ajili ya asili yake, ya jina lake, ya maoni yake, ya dini yake ao ajili ya hali yake ya maisha.

Kila mkongomani ana haki na mapashwa ya kushiriki, kupitia kwa kazi yake, kwa juhudi za kuijenga na kuistawisha taifa.

Sharia inabainisha jisimu ya wafanya kazi na kupanga kawaida za kipekee kuhusu makundi fulani ya kipekee ya wafanya kazi ao kanuni za matumikio ya kazi fulani fulani ambazo zinadai ujuzi na taaluma za kipekee.

Mipango ya ndani ya mashirika ya kikazi na mwenendo wayo vinapashwa kuheshimu kawaida za demokrasia.

Kifungo cha 37*a*

Serikali inazamini haki ya kuunda mashirika.

Viongozi watawala wanasharikiana na mashirika ya kipekee inayoshurulikia maendeleo ya kijamii, ya kiuchumi, ya kielimu, ya nafsi, na ya roho pamoja na maadibisho ya wananchi.

Mashirikiano haya yanaweza kuwa kwa sura ya msaada wa kifedha.

Sharia inabainisha jinsi ya kufaulu kwa haki hiyo.

Kifungo cha 38*e*

Uhuru wa kutetea wafanya kazi unajuzishwa na kuzaminiwa.

Wakongomani wote wana haki ya kuunda mashirika ya kuwatetea wafanya kazi na kujiunga kwa shirika la utetezi wanalolitaka kwa hiari, katika kuheshimu masharti ya sharia.

Kifungo cha 39*a*

Haki ya mgomo inajuzishwa na kuzaminiwa.

Haki hiyo inaendeshwa kufwatana na mipango ya sharia ambayo inaweza kuikataza ama kuizuwiya kiasi, kwa yanayohusu shuruli za kinga ya taifa, usalama na idara fulani fulani za serikali ambazo shuruli zake ni za muhimu sana kwa mwenendo wa maisha ya taifa nzima.

Kifungo cha 40*i*

Mtu yeyote ana haki ya kuowana na mtu mwengine wa jinsia mbalimbali na yake ambaye anamchagua mwenyewe na kuunda hivi jamaa lao.

Kama vile kiini ao msingi wa jumuiya ya walimwengu, jamaa inaundwa kwa jinsi ya kuimarisha mfungamano wake na kuistawisha yenyewe.

Jamaa inawekwa chini ya ulinzi na kinga ya serikali.

Ni haki yao ya kawaida na wajibu wao wazazi kuwahudumia watoto wao kwa matunzo na maadibisho, chini ya uchunguzi na kwa msaada wa serikali.

Watoto pia kwa upande wao wana mapashwa ya kuwasaidia wazazi wao.
Sharia inabainisha kawaida ya kufunga ndoa na kujenga jamaa.

Kifungo cha 41*a*

Huitwa mtoto mdogo mtu yeyote, bila tofauti ya jinsia, asiyekamilisha bado umri wa miaka kumi na minane (18) timamu.

Ni haki kwa kila mtoto mdogo kuyatambua majina ya baba yake na ya mama yake.

Ni haki yake pia kufaulu na kinga ya jamaa lake, ya jumuiya ya watu na ya serikali.

Kuwatelekeza na kuwatesa watoto wadogo, hasa kwa kuzini nao, kufanya biashara ya zina ya watoto, na kuwashutumu uchawi, vinakatazika kabisa na kuazibiwa vikali na sharia.

Ni mapashwa yao muhimu wazazi kuwatunza watoto na kuwakinga zidi ya matendo yote ya utesaji, ndani kama vile njee ya jamaa.

Ni wajibu wao viongozi watawala kuwakinga watoto katika hali ya magumu na kuwapeleka mahakamani hao wote wanaowatatiza watoto wadogo, pamoja na hao wanaoshirikiana nao.

Hali nyingine yoyote ya kuwatumia watoto wadogo kama vyombo zinaazibiwa vikali sana na sharia.

Kifungo cha 42*i*

Ni jukumu yao viongozi watawala kuwakinga vijana zidi ya hatia zote za kuleta mazara kwa afia yao, kwa maadibisho yao na kwa maendeleo ya nafsi zao.

Kifungo cha 43*u*

Kila mtu ana haki ya kupewa mafunzo kwa kupitia kwenyi masomo ya kitaifa.

Masomo ya kitaifa ni jumla ya shule na vyuo vya serikali, na hizo za kipekee zinazopewa kibali na serikali.

Sharia maalumu inapambanua jinsi ya kuunda na kuendesha shule na vyuo.

Ni mapashwa yao muhimu wazazi kuwachagulia watoto wao aina ya mafunzo inayowafaa.

Mafunzo ya msingi inalazimika kwa kila mtoto na haina ada yoyote kunako shule za serikali.

Kifungo cha 44*e*

Kukomesha na kutokomeza kabisa hali ya kutojua kusoma na kuandika ni mojawapo katika mapashwa muhimu ya taifa nzima ambayo inapangiliwa sera maalumu na serikali.

Kifungo cha 45*o*

Mafunzo yako huru.

Bali, yanawekwa chini ya uchunguzi wa serikali kwa mujibu wa sharia maalumu.

Mtu yeyote ana haki ya kujiandikisha kunako shule kufwatana na uwezo wake bila ya kubaguliwa kwa asili yake, kwa rangi yake, kwa dini yake, kwa jinsia yake, kwa msimamo wake wa kisiasa, kwa maoni yake ya kiimani, kwa hali yake ya mwili ao ya akili.

Shule za mafunzo za kitaifa zinaweza, kwa makubaliano na wakuu viongozi wa dini fulani na kwa maombi ya wazazi, kuwapa watoto wadogo mafundisho inayoafikiana na dini yao.

Viongozi watawala wanayo mapashwa ya kushurulikia na kukuza heshima ya haki za mwanaadamu, huru za msingi na mapashwa ya wananchi, kama inavyopangwa na katiba hii, kwa kupitia njia ya mafunzo, ya maadibisho na ya matangazo.

Inawahusu pia viongozi watawala kushurulikia kutangaza na kufundisha katiba ya jamhuri, tangazo la kimataifa kuhusu haki za mwanaadamu, mkataba wa kiafrika kuhusu haki za mwanaadamu na za nyumma, na mikataba mingine ya barani ao ya kimataifa kuhusu utekelezaji wa haki za mwanaadamu na sharia za mawasiliano ya kilimwengu ambayo imeizinishwa nchini.

Inahusu pia serikali kuingiza kunako ratiba ya mafunzo ya askari jeshi, ya askari polisi na ya maafisa wa usalama taratibu za heshima ya haki ya mwanaadamu.

Sharia inapambanua matumikio ya kifungo hichi.

Kifungo cha 46*a*

Haki za kitamaduni, uhuru wa ubunaji wa kimaarifa na wa kifundi, uhuru wa utafiti wa kisayansi na wa kiteknolojia

vinajuzishwa kwa wananchi wote katika kuheshimu sharia, mipango ya ukimya na mila mizuri.

Haki za mtenzi na ubinafsi wa maarifa ya muundaji zinazaminiwa na sharia.

Serikali inahusishwa, katika matumizi ya shuruli zake za kawaida, kutegamia pia uwingi wa matamaduni iliyoko nchini.

Kifungo cha 47*a*

Serikali ina jukumu ya kuhudumia afia na usalama wa raia kwa chakula.

Sharia inabainisha mipango ya msingi ya kuhudumia afia ya umma na usalama wa raia kwa chakula.

Kifungo cha 48*e*

Haki kwa kila mwananchi kuwa na makazi mazuri, kupelekewa maji masafi kwa kunywa na nguvu ya umeme, zinazaminiwa.

Sharia inafafanua mipango ya kutimiza haki hizo.

Kifungo cha 49*a*

Wakongwe na walemavu wana haki ya kuhudumiwa kwa hatua za kipekee za ukingo kuhusu shida zao za kiwiliwili, za kielimu na za kinafsi.

Ni jukumu yake serikali kuchochea waweko walemavu kunako vyumba mbalimbali vya uongozi wa taifa, wa majimbo na wa mitaa.

Sharia maalumu ya uongozi inafafanua jinsi ya kutumikisha haki hizo.

## KIPINDI CHA TATU
## HAKI ZA JUMUIYA

Kifungo cha 50/

Serikali inajukumishwa kukinga haki na faida halali ya raia wakongomani wote, waliomo nchini na hao wanaoishi njee ya Jamhuri.
Pamoja na haki ya kurudisha wanayotenda wengine zidi ya wakongomani wa nje, kila mgeni anayeishi kisharia ndani ya ardhi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo anahusika pia na haki na huru wanayofazilikiwa wakongomani, ila tu haki za kisiasa.

Anafaulu vilevile na kinga wanayopewa watu na mali yao kwa mipango inayobainishwa na sharia pia na makubaliano mengine.

Anahusika pia na kuheshimu na kutii sharia na kanuni zote za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kifungo cha 51*a*

Serikali inalazimika kushurulikia na kukuza mfungamano wa makundi mbalimbali ya raia.

Inahusika pia na ukingo na maendeleo ya makundi ya wazalili na walio wachache.

Inashurulikia maendeleo yao.

Kifungo cha 52*i*

Ni haki yao wakongomani wote kujaliwa amani na usalama ndani ya mipaka ya nchi kama vile njee.

Haijuzu hata kidogo mtu yeyote, ao kundi fulani la watu, kutumia sehemu fulani ya ardhi ya taifa kuwa msingi ao chanzo cha matendo ya uhasi, ya usaliti ao ya ugaidi zidi ya serikali ya Kongo ao zidi ya serikali ya nchi nyingine yoyote.

Kifungo cha 53*u*

Kila mtu ana haki ya kufaulu kwa mazingira masafi inayorahisisha maendeleo ya nafsi yake.

Anayo pia mapashwa ya kuikinga mazingira.

Serikali kwa upande wake inahusika na kushurulikia ukingo wa mazingira pamoja na afya ya raia.

## Kifungo cha 54*e*

Masharti ya kujenga viwanda, ya kurundika, kutumia, kuunguza na kusafirisha makamvi ya kinuklea na ya bizaa nyingine inayoweza kuleta mazara kwa afya ao kuchafua mazingira, kutoka kwenyi viwanda ao mitambo mingine ya kifundi iliyoko ndani ya nchi, inabainishwa na sharia.

Machafuzi yoyote ya mazingira ao ubomoaji wowote unaosababishwa na shuruli fulani ya kiuchumi, inalipizwa faini.

Sharia inafafanua kiwango na hali ya faini pia na namna ya malipo yake.

## Kifungo cha 55*o*

Kusafirisha kwa kupitia nchini, kuagiza kutoka njee, kurundika, kuzika ama kumwagilia ndani ya maji iliyomo nchini, ao ndani ya sehemu ya mabahari iliyo chini ya utawala wa Kongo, kama

vile kunyunyuzia ndani ya anga ya Kongo makamvi yoyote inayoweza kuleta mazara kwa afya ya watu, inayoweza kuchafua mazingira, ya kinuklea ao ya aina nyingine yoyote, kutoka njee ao laa, ni hatia kubwa inayoazibiwa vikali na sharia.

Kifungo cha 56*a*

Bila kuhasiri mipango ya kimataifa kuhusiana na hatia za kiuchumi, kitendo chochote, makubaliano yoyote ao jambo lolote ambalo matokeo yake ni kuipotezea taifa, ao watu binafsi, ao tena shirika fulani, jumla ao sehemu ya mapato yake ya kujifaidia kutokana na rasilimali zake za kawaida, ni hatia inayofananishwa na hiyo ya kupora mali na kuazibiwa vikali na sharia.

Kifungo cha 57*a*

Matendo yanayotajwa kunako kifungo kinachotangulia, pamoja na jaribio lolote la kuyatenda, bila kutizama mipangilio yake, yanahusiana na hatia ya usaliti, ikiwa kama anayeshutumiwa ni mtu anayeshikilia madaraka fulani ya utawala.

Kifungo cha 58*e*

Wakongomani wote kwa jumla wana haki ya kufaulu na utajiri wa nchi yao.

Ni juu ya serikali wajibu wa kugawa kwa uadilifu utajiri huo na kuhudumia haki ya maendeleo.

Kifungo cha 59*a*

Wakongomani wote kwa jumla wana haki ya kufaulu na rasilimali ya jumuiya ya walimwengu.

Ni juu yake serikali jukumu ya kuwarahisishia fazila hiyo.

Kifungo cha 60*i*

Kuheshimu haki na huru za msingi za mwanaadamu kama zinazosibitishwa na katiba hii ni mkazo juu ya viongozi watawala na juu ya kila mtu.

Kifungo cha 61*a*

Kwa hali yoyote, hata kama inatangazwa hali ya wasiwasi ama ya zarura kufwatana na vifungo vya 87 na 88 vya katiba hii, haiwezi hata kidogo kutenguliwa haki na mipango ya msingi inayofwata, yaani :

1. Haki ya maisha;
2. kikatazo cha utesaji na cha azabu ama matendo ya utesaji, isiyokuwa ya kiutu na ya kupunguza heshima ya mtu;

3. kikatazo cha utumwa na hali ya kuheshimu sharia katika kupanga hatia na azabu zake;
4. haki ya kujitetea na ya rufaa;
5. kikatazo cha kifungo ajili ya deni;
6. uhuru wa fikara, wa zamiri na wa dini.

## KIPINDI CHA NNE
## KUHUSU MAPASHWA YA RAIA

### Kifungo cha 62*i*

Hayuko mtu yeyote anayezaniwa kutotambua sharia.

Mtu yeyote analazimishwa kuheshimu katiba na sharia za Jamhuri.

### Kifungo cha 63*u*

Ni juu ya kila mkongomani haki na mapashwa ya kukinga nchi katika mipaka yake zidi ya hatari na uvamizi kutoka njee.

Vijana wanaweza kupewa kwa shuruti mafunzo ya kijeshi kufwatana na masharti inayobainishwa na sharia.

Ni mapashwa muhimu kwa yule yote anayeshikilia madaraka ya utawalo wa taifa, wa jimbo, wa mitaa, hadi wa mikoa na maeneo ya usultani wa asili, kutetea muungano wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kukinga mipaka yake. Bila hivo atashutumiwa usaliti.

Kifungo cha 64*e*

Kila mkongomani ana haki ya kumzuwiya mtu yeyote, ama kundi lolote la watu, anayechukuwa mamlaka kwa nguvu ao anayetawala kinyume na mipango ya katiba hii.

Jaribio lolote la kuipindua serikali iliyohalalishwa na katiba, ni hatia zidi ya taifa na serikali yake, isiyokuwa na mda kwa kuamuliwa, na inaazibiwa kufwatana na sharia.

Kifungo cha 65*o*

Ni juu yake kila mkongomani wajibu wa kutimiza kwa uadilifu mapashwa yake mbele ya serikali.

Mapashwa hayo ni pamoja na kulipa kodi na nyushuru zingine.

Kifungo cha 66*a*

Kila mkongomani anapashwa kuheshimu wananchi wenzake na kuishi nao bila ubaguzi wowote. Ni juu yake pia kukuza na

kuimarisha muungano wa taifa, heshima na ustahamilivu baina yake na wananchi wenzake.

Anayo pia mapashwa ya kukinga na kuimarisha mfungamano wa kitaifa, hususa wakati unahatarishwa.

Kigungo cha 67*a*

Kila mkongomani analazimishwa kukinga rasilimali, mali na faida za jumuiya na kuheshimu kabisa mali za wengine.

## MLANGO WA TATU
## MIPANGILIO YA UTAWALA

### KIPINDI CHA KWANZA
### VYUMBA VYA UTAWALA WA JAMHURI

Kifungo cha 68*e*

Vyumba vya utawalo wa Jamhuri ni vifwatavyo :

1. Rais wa Jamhuri;
2. B u n g e;

3. Serikali;
4. Korti na Mahakama.

SEHEMU YA KWANZA : VYUMBA VYA UTAWALA

FUNGO LA KWANZA : RAIS WA JAMHURI

Kifungo cha 69*a*

Rais wa Jamhuri ndio kiongozi wa nchi. Anawakilisha taifa pamoja na kuwa ishara ya muungano wa taifa.

Rais wa Jamhuri analingania utekelezaji wa katiba.

Anasimamia kwa hekima yake mwenendo kawaida wa vyumba na idara mbalimbali ya serikali pamoja na mfululizo wa kazi za serikali.

Ni yeye pia mzamini wa uhuru wa taifa, wa utimamu wa ardhi, wa enzi ya taifa na wa utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa.

Kifungo cha 70*i*

Rais wa Jamhuri anachaguliwa moja kwa moja kwa kura ya wananchi kwa muhula wa miaka mitano unaoweza kurudiliwa mara moja tu.

Ukimalizika mda wake, Rais anabaki kuendesha kazi zake hadi pale atapotawazishwa rasmi Rais mchaguliwa wa sasa.

Kifungo cha 71*a*

Anachaguliwa Rais wa Jamhuri mgombea anayetimiza uwingi wa kura inayozidi asili mia hamsini ya jumla ya sauti za waliopiga kura.

Ikiwa kama haukupatikana uwingi huo kwa duru ya kwanza, inapangwa na kuendeshwa duru ya pili baada tu ya siku kumi na tano.

Hawahusike na duru hiyo ya pili ila wagombea wawili waliojinyakulia sauti nyingi kuliko wengine kunako duru ya kwanza.

Kukitokea kifo ao kizuwizi kwa mgombea moja anayehusika na duru ya pili, ao akajiondoa mwenyewe katika kinyanganyiro, basi atashiriki anayemfwata kwa idadi ya sauti katika kuheshimu jinsi walivopangana kunako duru ya kwanza.

Anatangazwa mshindi wa uchaguzi wa Rais baada ya duru ya pili, mgombea ambae atakusanya sauti zaidi ya mpinzani wake.

Kifungo cha 72*i*

Hakubaliwi yeyote kugombea uchaguzi wa Rais wa jamhuri ikiwa hatimize sifa zifwatazo :

1. Kuwa mkongomani wa asilia;
2. Kuwa, kwa uchache, na miaka salasini (30) ya kuzaliwa;
3. Kuwa na haki kamili za kiraia na za kisiasa;
4. Kutopatikana na mojawapo kati ya vizuwizi vinavyopangwa na sharia ya uchaguzi.

Kifungo cha 73*u*

Kura ya kumchagua Rais mpya wa Jamhuri inapangwa na kuendeshwa na Tume ya uchaguzi siku tisini (90) kabla umalizike mda wa Rais aliye madarakani.

Kifungo cha 74*e*

Rais mchaguliwa anachukua madaraka yake siku kumi (10) baada ya kutangazwa rasmi matokeo ya mwisho ya kura.

Kabla aanze kazi, Rais wa Jamhuri anaapa mbele ya Korti Kuu ya Katiba kiapo kisemacho :

*“Mimi (Fulani Bin Fulani), niliyechaguliwa Rais wa “Jamhuri, naapa leo zahiri, mbele ya M.Mungu na mbele “ya taifa nzima :*

*“- kutekeleza na kuheshimu katiba na sharia za Jamhuri;*

*“- kulingania uhuru wake na kukinga mipaka yake;*

*“- kukinga muungano wa taifa;*

*"- kutotetea ila tu faida ya umma na heshima ya haki za mwanaadamu;* "

*"- kujitolea kwa nguvu zangu zote na kwa uwezo wangu wote kwa kuboresha maisha na kukuza amani;* "

*"- kutimiza kwa uhaki, kama vile mtumishi amini wa raia na wa umma, kazi hii kubwa ninayopewa."* "

Kifungo cha 75*o*

Kukitukia kifo cha Rais, ama akajiuzulu mwenyewe, ama tena akikabiliwa na kizuwizi kingine kinachosababisha ashindwe kabisa kuendesha kazi zake, mamlaka ya Rais wa Jamhuri inashikiliwa kwa mda na Prezidenti wa Seneti, isipokuwa tu hiyo ya kipekee inayoagizwa kunako vifungo vya 78, 81 na 82 (vya Katiba hii).

Kifungo cha 76*a*

Hali ya kukosekana Rais inatangazwa na Korti Kuu ya Katiba kwa kupelekewa habari rasmi na serikali.

Rais wa mda anashurulikia hasa kupanga uchaguzi wa Rais mpya kwa mda na kufwatana na masharti inayobainishwa na Katiba.

Ikibaki wazi nafasi ya Rais ao kikitangazwa na Korti Kuu ya Katiba kizuwizi cha kudumu zidi ya Rais, uchaguzi wa Rais mpya utaitishwa na Tume Huru ya Uchaguzi kwa kipindi cha

siku isiyopungua sitini (60), kwa uchache, wala isiyozidi tisini (90), kwa uwingi, kinachofwatia tangazo rasmi ya kizuwizi cha Rais.

Kukitukia jambo la zarura, mda huo unaweza kuongezwa na Korti Kuu ya Katiba hadi siku mia na ishirini (120), bila zaidi, kwa pendekezo la Tume Huru ya Uchaguzi.

Rais mchaguliwa anaanza muhula wake mwengine.

Kifungo cha 77*a*

Rais wa Jamhuri anawasiliana na umma kwa njia ya hutuba.

Anawasiliana na vyumba vya Bunge kwa njia ya nyaraka anazozisoma mwenyewe ama zinazosomwa na mwengine ambazo hazihusike na mjadala wowote.

Mara moja kwa mwaka, anahutubia Chumba cha wateule na Seneti vikikusanyika pamoja katika Kongresi, kuhusu hali ya taifa.

Kifungo cha 78*e*

Rais wa Jamhuri anamteuwa Waziri Mkuu kutoka kwa kikundi kilicho na wateule wengi kunako Bunge, baada ya kuhojiana na kikundi chenyewe.

Na anamuachisha kazi pale tu huyo atampelekea hati ya kuuzulu serikali.

Ikiwa hakipatikane kikundi cha wateule wengi kunako Bunge, Rais wa Jamhuri atamteuwa mtu fulani na kumpa kazi ya kugundua hao katika Bunge wanaoafikiana.

Mda wa kazi ya mtu huyo hauzidi siku salasini (30) inayoweza kurudiliwa mara moja tu.

Rais wa Jamhuri atawateuwa memba wengine wa serikali na kuwaachisha kazi kwa pendekezo la Waziri Mkuu.

Kifungo cha 79*a*

Rais wa Jamhuri anaitisha na kuongoza mikutano ya Baraza la mawaziri. Akizuwiliwa na shida, anawakilishwa na Waziri Mkuu.

Rais wa Jamhuri anaizinisha sharia kwa mpango unaobainishwa na katiba hii.
Anachukua hatua mbalimbali kwa njia ya AMRI za Rais.

Amri za Rais, isipokuwa tu zile zinazoagizwa na vifungo vya 78, sehemu yake ya kwanza, 80, 84 na 143, zinatiwa sahihi na Waziri Mkuu.

Kifungo cha 80*i*

Rais wa Jamhuri anawatawazisha kwa njia ya amri yake maliwali wa majimbo na makamu wao kwa mda usiozidi siku 15 tangu kuchaguliwa kwao kufwatana na kifungo cha 198.

Kifungo cha 81*a*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba, Rais wa Jamhuri ndie anawateuwa na kuwavuwa madaraka, hata ikiwezekana, kuwaachisha kazi kwa pendekezo la serikali lililojadiliwa na baraza la mawaziri :

- mabalozi na wajumbe wa kipekee;
- majemadari na maafisa wakuu wa jeshi na wapolisi, baada ya mahojiano na baraza kuu la ulinzi;
- kamanda mkuu wa jeshi na makamanda wa vikosi mbalimbali vya jeshi, baada ya kuihoji baraza kuu la ulinzi;
- maafisa wa ngazi ya juu kunako idara za serikali;
- viongozi wa taasisi za serikali;
- wakuu viongozi wa mashirika ya serikali na mitandao mingine ya serikali, isipokuwa hao wanaohusika na uchunguzi wa matumizi ya pesa.

Amri za Rais za kuteuwa, kuvua madaraka na kuachisha kazi viongozi hao, zinatiwa sahihi na Waziri Mkuu.

Kifungo cha 82*i*

Rais wa Jamhuri anawateuwa, anawavua madaraka, hata ikiwezekana, anawaachisha kazi kwa njia ya amri zake, wanasharia kunako vituo mbalimbali na vyumba vya mahakama na vya wakata mashataka wa serikali kwa pendekezo la Halmashauri Kuu ya Uamzi.

Amri zake kuhusu mipango hiyo zinatiwa sahihi na Waziri Mkuu.

Kifungo cha 83*u*

Rais wa Jamhuri ndie Kamanda Mkuu wa majeshi.
Anaongoza vikao vya Baraza Kuu la ulinzi.

Kifungo cha 84*e*

Rais wa Jamhuri ndie anavika vyeo na kuwatunukia watu kwa nishani ya heshima kwa mujibu wa sharia.

Kifungo cha 85*o*

Ikitukia hali fulani inayohatarisha kwa karibu kabisa uhuru na mipaka ya nchi ama kukatiza rafla mwenendo wa vyumba vya

serikali, Rais wa Jamhuri anatangaza hali ya wasiwasi ao hali ya zarura baada ya kuhojiana na Waziri Mkuu na maprezidenti wa vyumba viwili vya Bunge, kufwatana na vifungo vya 144 na 145 vya Katiba hii.

Anawajulisha raia kwa njia ya hutuba.

Sharia inabainisha na kufafanua mipango ya kuendesha mambo wakati wa hali ya wasiwasi ao wakati wa zarura.

Kifungo cha 86*a*

Rais wa Jamhuri anaamuru vita kwa amri yake iliyojadiliwa na baraza la mawaziri baada ya kuihoji baraza kuu ya ulinzi na kuiziniwa na Vyumba viwili vya bunge, kufwatana na kifungo cha 144 cha katiba hii.

Kifungo cha 87*a*

Rais wa Jamhuri ndie ana haki ya msamaha.

Anao uwezo wa kufuta, kubadili ao kupunguza azabu.

Kifungo cha 88*e*

Rais wa Jamhuri ndie anatuma na kukubalisha mabalozi na wajumbe wa kidiplomasia kunako nchi za kigeni na mashirika ya kimataifa.

Ni kwake pia ndio wanatumwa na kukubalishwa mabalozi na wajumbe wa nchi nyingine.

Kifungo cha 89*a*

Ujira na oroza ya matumizi ya Rais wa Jamhuri vinapangwa na sharia ya mali.

FUNGO LA PILI : YANAYOHUSU SERIKALI

Kifungo cha 90*i*

Serikali inaundwa na Waziri Mkuu na mawaziri na mawaziri makamu, ao pengine na Mawaziri Wakuu makamu, mawaziri wa serikali na mawaziri wajumbe.

Serikali inasimamiwa na Waziri Mkuu, aliye pia kiongozi wa serikali. Akipatikana na kizuwizi, waziri mkuu anawakilishwa na memba wa serikali aliye na daraja ya juu kuliko wengine.

Katika kuundwa kwake serikali itatezama pia uwakilishi wa taifa nzima.

Kabla aanze kazi, Waziri Mkuu anaonyesha kwenyi Bunge sera ya serikali yake.

Ikiwa sera hiyo itakubaliwa kwa uwingi wa kawaida wa wateule, yaani zaidi ya nusu kati ya wateule, hapo baraza ya wateule inamtawazisha waziri mkuu.

Kifungo cha 91*a*

Kwa makubaliano na Rais wa Jamhuri, serikali inapanga siasa ya taifa na kubeba jukumu yake.

Serikali inaongoza siasa ya taifa.

Ama kuhusu ulinzi, usalama na mambo ya kigeni, hivyo vinaendeshwa kwa maafikiano kati ya Rais wa Jamhuri na serikali.

Serikali inamiliki idara za serikali, jeshi, polisi na idara za usalama.

Serikali inajukumika mbele ya Chumba cha wateule kwa mipaka inayopangwa na vifungo vya 90 na 100.

Amri ya Rais inayojadiliwa na baraza la mawaziri inabainisha mipango na uendeshaji wa serikali pia na hali ya mawasiliano kati ya Rais wa Jamhuri na serikali, na kati ya memba wa serikali wao kwa wao.

Kifungo cha 92*i*

Waziri Mkuu ndie anahusika na kutumikisha sharia na anashikilia uwezo wa kupanga kanuni bila kuhasiri mamlaka anayopewa Rais wa Jamhuri na katiba hii.

Anaongoza kwa njia ya dikrii.

Anateuwa kwa dikrii viongozi na watumishi wa kazi mbalimbali za serikali na jeshi kwa daraja isiyomhusu Rais wa Jamhuri.

Mara kwa mara, hatua za Waziri Mkuu zinatiwa sahihi na mawaziri wanaohusika na utendaji wake.

Waziri Mkuu anaweza kuwapa mawaziri sehemu ya mamlaka yake.

Kifungo cha 93*u*

Waziri ndio kiongozi wa wizara yake.
Anahusika na kuendesha sera ya serikali kwa yanayohusu wizara yake, chini ya uongozi wa waziri mkuu.

Anaongoza kwa njia ya HATUA ya Waziri.

Kifungo cha 94*e*

Mawaziri makamu wanahusika na kuendesha, chini ya mamlaka ya mawaziri wao, shuruli wanazopewa na amri kuhusu mpango na mwendo wa serikali.

Wanawawakilisha mawaziri wao wakikosekana ao wakiwa na kizuwizi.

Kifungo cha 95*o*

Ujira wa memba wa serikali unabainishwa na sharia ya mali.

Waziri Mkuu anapewa, zaidi ya ujira, mfuko fulani kwa matumizi.

## FUNGO LA TATU : MIPANGO YA JUMLA KUHUSU RAIS WA JAMHURI NA SERIKALI

Kifungo cha 96*a*

Wazifa wa Rais wa Jamhuri haumruhusu kuchanga na awamu nyingine yoyote ya uteule, ama kufanya kazi nyingine yoyote ya uraia ama katika jeshi, ao shuruli zingine za kikazi.

Haumruhusu pia kushikilia madaraka yoyote katika chama cha siasa.

Kifungo cha 97*a*

Wazifa wa memba wa serikali haumruhusu anaoushikilia kuchanga na awamu nyingine yoyote ya uteule, ama kufanya kazi yoyote ya uraia ama katika jeshi, ao shuruli zingine za kikazi.

Haumruhusu pia kushikilia madaraka yoyote katika chama cha siasa.

Kifungo cha 98*e*

Kwa mda wowote wa kazi yao, Rais wa Jamhuri na memba wa serikali hawaruhusiwi, kwa wao wenyewe ao kwa niaba ya mtu mwengine, kununua ao kujipatia kwa njia yoyote, wala kukodi kitu kinachojulikana kuwa mali ya serikali, ya majimbo ao ya maeneo inayojitawala.

Hawawezi kushiriki moja kwa moja, ao kwa njia ya wakili, katika mikakati ya masoko fulani inayohusiana na faida ya idara ao vyumba vya serikali kuu, vya majimbo ao maeneo inayojitawala.

Kifungo cha 99*a*

Mwanzo na mwisho wa kazi yao, Rais wa Jamhuri na memba wa serikali wanalazimika kupeleka mbele ya Korti Kuu ya Katiba oroza ya mali na rasilimali zao na za familia yao, ikiwemo vyombo na vifaa, vidamu na michango kunako mashirika, vifaa vya samani, akiba kwenyi benki, majumba, hata viwanja visivojengwa, sehemu ya ardhi na za misitu, mashamba na ardhi ya kulima, mashimo ya madini, na kubainisha uhakika wa kila kile.

Mali na rasilimali za familia inahusisha pia mali ya ndoa yake, ya watoto wake wadogo, hata hao wanaobalehe walioko chini ya usimamizi wa ndoa yao.

Korti Kuu ya Katiba itaituma oroza hiyo mbele ya taasisi ya ushuru.

Ikikosekana oroza hiyo mda wa siku salasini (30), anayehusika atakuwa kama anajiuzulu.

Ikikosekana kwa siku salasini (30) inayofwatia kumalizika kipindi cha kazi, ao ikiwa italetwa oroza ya udanganyifu, ao tena kwa shutuma ya kutajirika kwa njia isiyokuwa halali, Korti Kuu ya Katiba ao Mahakama Kuu itachungulia jambo hilo.

## SEHEMU YA PILI : UWEZO WA KUTUNGA SHARIA

### Kifungo cha 100*a*

Uwezo wa kutunga sharia ni juu ya Bunge ambayo ina vyumba viwili, yaani Chumba cha wateule na Seneti, ama chumba cha Wazee.

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, Bunge ndio inahusika na kuwafiki sharia mbalimbali, pamoja na kuchunguza kazi za serikali, mashirika, idara na taasisi zote za serikali.

Kila chumba kina uhuru wa kujiendesha na wa matumizi ya mali na kina hazina yake ya pekee.

## FUNGO LA KWANZA : KUHUSU CHUMBA CHA WATEULE

### Kifungo cha 101*a*

Memba wa chumba cha wateule huitwa wateule wa taifa. Wanachaguliwa moja kwa moja kwa kura ya siri ya raia.

Wagombea wanawakilishwa na vyama ao mashirika mbalimbali ya kisiasa. Anaweza pia kujitokeza mgombea wa kibinafsi.

Kila mteule wa taifa anachaguliwa na makamu wake wawili.

Mteule wowote anawakilisha taifa nzima.

Mkazo kwa mteule kulingania ila kuli hali msimamo wa chama fulani unaharamishwa kabisa.

Idadi jumla ya wateule wa taifa, namna ya kuchaguliwa kwao pamoja na sifa za wagombea, vinaashiriwa na sharia ya uchaguzi.

## Kifungo cha 102*i*

Hawezi kuwakilishwa ama kujitokeza mtu kuwa mgombea kwenyi uchaguzi wa wateule, ila akikusanya masharti yafwatayo :

- Kuwa mkongomani;
- Kuwa, kwa uchache, na umri wa miaka 25 ya kuzaliwa;
- Kuwa na utimamu wa haki za uraia na za kisiasa;
- Kutojikuta na mmojawapo katika vitengamizi vinavyotiwa na sharia ya uchaguzi.

## Kifungo cha 103*u*

Mteule wa taifa huchaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano. Ana haki ya kuchaguliwa tena.

Mda wa kipindi cha mteule wa taifa unaanza kuhisabiwa hapo utakubaliwa uwezo wake na chumba cha wateule na kumalizika kitaposimikwa chumba kingine cha wateule.

## FUNGO LA PILI : KUHUSU SENETI

### Kifungo cha 104*e*

Memba wa chumba cha seneti huitwa mwanaseneti.

Mwanaseneti anawakilisha jimbo lake, ilakini awamu yake ni ya kitaifa.

Wagombea wanawakilishwa na vyama ao makundi mbalimbali ya kisiasa. Anaweza pia kujitokeza mgombea wa kibinafsi.

Kila mwanaseneti anachaguliwa na makamu wake wawili.

Marais wa Jamhuri wastahifu waliochaguliwa wanapewa fazila ya kuwa wanaseneti kwa maisha yao mazima.

Idadi jumla ya wanaseneti, mipango ya kuchaguliwa kwao na sifa za wagombea, vinaashiriwa na sharia ya uchaguzi.

### Kifungo cha 105*o*

Mwanaseneti huchaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano. Ana haki ya kuchaguliwa tena.

Mda wa kipindi cha mwanaseneti unaanza kuhisabiwa hapo utakubaliwa uwezo wake na chumba cha seneti na kumalizika kitaposimikwa chumba kingine kipya cha seneti.

Kifungo cha 106*a*

Hawezi kuwakilishwa ao kujitokeza mtu kuwa mgombea uchaguzi wa wanaseneti ila anayekusanya masharti yafwatayo :

- Kuwa mkongomani;
- Kuwa, kwa uchache na umri wa miaka salasini (30) ya kuzaliwa;
- Kuwa na utimamu wa haki za uraia na za kisiasa;
- Kutojikuta na mmojawapo katika vitengamizi vinavyotiwa na sharia ya uchaguzi.

FUNGO LA TATU : KUHUSU HIFAZI NA USAMBAMBA

Kifungo cha 107*a*

Mbunge yeyote hawezi kushtakiwa, kusagwa, kuzuwiliwa, kufungwa ama kuhukumiwa kutokana na maoni ao na msimamo wake ama kuhusiana na kura wakati wa kazi zake kwenyi Bunge.

Wakati wa vikao, mbunge hawezi kushtakiwa ao kuzuwiliwa ila kwa ruhusa ya chumba cha wateule ao ya seneti, ao kwa

fumanizi, ao tena kwa mashtaka iliyokwisharuhusiwa ama kwa hukumu iliyokwishakatwa.

Kifungo ama mashtaka inayomkabili mbunge, inaweza kusimamishwa kwa maombi ya chumba aliko memba, kwa mda usiozidi kipindi cha kikao kinachoendeshwa bungeni.

Kifungo cha 108*e*

Hawezi mtu kuwa mara moja mteule wa taifa na mwanaseneti, ao tena, kwa kupindua, kuwa mwanaseneti na mteule wa taifa.

Kazi ya mteule wa taifa na ya mwanaseneti hairuhusiwe hata kidogo kuchanganywa na kazi ama shuruli zingine zifwatazo :

- memba wa serikali;
- memba wa vyumba vya kulingania demokrasia;
- askari jeshi, askari polisi ao afisa wa idara ya usalama;
- hakimu ama jaji ao mkata mashtaka wa serikali;
- mtumishi kunako idara za serikali;
- mkuu kiongozi wa jimbo ao wa maeneo mengine, isipokuwa tu sultani wa asili;
- wakili wa serikali;
- memba wa chumba cha kazi cha Rais wa jamhuri, cha Waziri Mkuu, cha Prezidenti wa chumba cha Wateule, cha Prezidenti wa seneti, cha memba wa serikali ao, kwa jumla, cha kiongozi wowote anayeshikilia wazifa wa utawalo; mtumishi kunako mashirika ya serikali, ao kunako shirika ya mchanganyiko wa mali;

- kazi zingine zozote za kuteuliwa.

Kazi ya mteule wa taifa na ya mwanaseneti haiende pamoja na kazi nyingine yoyote ya kuajiriwa na nchi nyingine ya kigeni ao na mashirika ya kimataifa.

## FUNGO LA NNE : HAKI ZA WATEULE WA TAIFA NA ZA WANASENETI

### Kifungo cha 109*a*

Wateule wa taifa na wanaseneti wana haki ya kutembea bila kizuwizi wala buguza yoyote ndani ya eneo nzima ya Jamhuri, hata kutoka njee.

Wanapewa ujira wa kutosha kwa nia ya kuzamini uhuru wao na hazi yao. Ujira huo unapangwa na sharia ya mali.

Mwisho wa mda wao wanapewa tuzo la mwisho linalolingana na miezi sita ya mshahara wao wa kawaida.

Mipango ya kutimiza yanayozungumzwa na sehemu inayotangulia ya kifungo hichi inaashiriwa na kawaida ya ndani ya kila chumba.

## FUNGO LA TANO : MWISHO WA KAZI YA MTEULE WA TAIFA NA YA MWANASENETI

### Kifungo cha 110*i*

Kazi ya mteule wa taifa na ya mwanaseneti inamalizika :

- Kwa kufikia mwisho wa mda wake;
- Kwa kifo;
- Kwa kujiuzulu;
- Kwa kizuwizi cha kudumu;
- Kwa uzaifu wa mwili;
- Kwa kukosekana bila sababu yoyote katika zaidi ya robo ya mikutano ya kikao;
- Kwa kufukuzwa kufwatana na mipango iliyoagizwa na sharia ya uchaguzi;
- Kwa kukubali kazi isiyoenda pamoja na kazi ya mteule wa taifa ao ya mwanaseneti;
- Kwa kuhukumiwa na sharia kwa azabu ya kifungo kufwatana na hatia ya kukusudia.

Kipingamizi chochote cha kuchaguliwa ambacho kitabainishwa baadae na afisa wa sharia anayehusika, kinavunja kazi ya mteule wa taifa ao ya mwanaseneti.

Hapo atagombolewa na makamu wake wa kwanza.

Mteule wa taifa ao mwanaseneti yeyote anapoteza nafasi yake kwenyi Bunge pale tu atajiuzulu kutoka kwa chama kilichomuwakilisha, hata ikiwa kati ya kipindi chake.

## FUNGO LA SITA : UENDESHAJI WA CHUMBA CHA WATEULE NA WA SENETI

### Kifungo cha 111*a*

Chumba cha wateule na seneti vinaongozwa, kila kile, na kamati ya uongozi ya memba saba wakiwemo :

- Prezidenti mmoja;
- Makamu Prezidenti wa kwanza
- Makamu Prezidenti wa pili;
- Katibu Mripoti mmoja
- Makamu Katibu mripoti;
- Mchunguzi wa feza mmoja
- Makamu mchunguzi wa feza mmoja.

Maprezidenti wa vyumba vyote viwili wanapashwa kuwa wakongomani wa asilia.

Memba wa kamati ya uongozi huchaguliwa kufwatana na masharti inayopangwa na kawaida ya ndani ya kila chumba.

Kifungo cha 112*i*

Kila chumba cha bunge kinapanga kawaida yake ya ndani ambayo inabainisha :

a. mda na kanuni ya uendeshaji wa kamati ya uongozi, mamlaka na mipaka ya uwezo wa prezidenti wake;
b. idadi ya kamisheni za chumba, namna ya kuteuwa memba wa kamisheni, ikiwemo pia kamisheni maalumu na ya mda;
c. mipango ya taasisi ya uendeshaji ya ndani ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa idara ya serikali, mmoja kwa kila chumba;
d. mipango ya kulinda adabu na kuazibu makosa ya wateule na wanaseneti;
e. namna mbalimbali ya kupiga kura, kuondoa tu hiyo inayofafanuliwa na katiba.

Kabla itumikishwe kawaida ya ndani, inatumwa na Prezidenti wa chumba kinachohusika mbele ya Korti Kuu ya Katiba kwa kukubalisha usambamba wake na Katiba kwa mda usiozidi siku 15. Ukizidi mda huo, kawaida hiyo itaonekana kama haiende kinyume na katiba.

Vifungo vya kawaida vitavyoonekana kwenda kinyume na katiba vitabatilishwa na kupigwa marufuku.

Kifungo cha 113*u*

Licha ya kamisheni za kudumu na hizo za pekee, vyumba vyote viwili vya Bunge, ikiwa vitahitilafiana kuhusu jambo ambalo vinahusika kutoa hatua moja kwa matamshi inayofanana, vinaweza kuunda kamisheni ya pamoja kwa kuzamia na kutatua hitilafu hiyo.

Ikiwa itashindikana kabisa, basi ni juu yake chumba cha wateule kujadili na kutoa hatua ya mwisho.

Kifungo cha 114*e*

Kila chumba cha Bunge kinakutana kwa sharia kwa kikao cha zarura siku 15 inayofwatia matangazo ya matokeo rasmi ya uchaguzi wa bunge na Tume Huru ya Uchaguzi kwa mazumuni ya :

a. Kuunda kamati ya mda itayoongozwa na mbunge aliye na umri zaidi ya wengine akisaidiwa na wabunge wawili walio na umri mdogo zaidi ya wengine.
b. Kuizinisha uwezo wa wabunge;
c. Kuchagua na kutawazisha kamati ya uongozi;
d. Kutunga na kuwafiki kawaida ya ndani.

Kikao hichi kinavipa nafasi vyumba vyote viwili kukutana kwa jinsi ya kutunga na kuwafiki kawaida ya ndani ya Kongresi.

Kikao hichi cha zarura kinajifunga pale tu itamalizika mambo iliyopangwa kunako agenda yake ya kazi.

Kifungo cha 115*o*

Kisharia, chumba cha wateule na seneti vinafanya, kila kile, vikao viwili vya kawaida kila mwaka.

- Kikao cha kwanza kinafunguliwa machi 15 na kumalizika yuni 15;
- Kikao cha pili kinafunguliwa septemba 15 na kumalizika desemba 15.

Ikiwa tarehe hizi za kufunguliwa kwa vikao zinaanguka jumapili ao siku kuu, kikao kinafunguliwa siku ya kwanza ya kazi inayofwatia.

Mda wa kila kikao cha kawaida hauzidi miezi mitatu.

Kifungo cha 116*a*

Kwa maoni ya kamati ya uongozi ao kwa maombi ya nusu kati ya memba wake, ya Rais wa Jamhuri ao ya Waziri Mkuu, Prezidenti wa kila chumba cha Bunge anaweza kuitisha kikao cha zarura kwa kujadili mambo fulani muhimu inayobainishwa.

Kikao hichi kinatanduka pale tu kinamaliza agenda ya mambo iliyokikutanisha, kwa mda usiozidi siku salasini (30).

Kifungo cha 117*a*

Unajuzishwa umuhimu wa kuandika kwenyi agenda ya kazi ya kila chumba pendekezo ya sharia ao muswada wa kwanza wa sharia, ao tena hutuba ya siasa ya jumla, ikiwa itaombwa na serikali baada ya kujadiliwa na baraza ya mawaziri.

Kifungo cha 118*e*

Vikao vya Chumba cha wateule na hivyo vya seneti havihalalike ila wakikutana memba kwa uwingi wa kawaida, yaani zaidi ya asili mia hamsini (50%).

Vikao vyote vinafanyika hazarani, isipokuwa tu ikitangazwa faraga.

Ripoti zote za mihazara na sahifa nyingine yote kuhusu Chumba cha wateule na hicho cha seneti zinatangazwa kunako gazeti ya matukio ya Bunge.

Kifungo cha 119*a*

Vyumba vyote viwili vya Bunge vinakutana pamoja kwa vikao viitwavyo Kongresi kwa umuhimu wa mambo yafwatayo :

- mpango wa kurekebisha katiba kwa mujibu wa vifungo 218 hadi 220 vya katiba hii;
- kutoa kibali cha kutangaza hali ya wasiwasi ao hali ya zarura ama cha kuamrisha vita kwa mujibu wa vifungo 85 na 86 vya katiba hii;
- kusikiliza hutuba ya Rais wa Jamhuri kuhusu hali ya taifa, kwa mujibu wa kifungo cha 77 cha katiba hii;
- kuwateuwa memba watatu wa Korti Kuu ya Katiba, kwa mujibu wa kifungo cha 158 cha katiba hii.

Kifungo cha 120*i*

Kinapokutana kikao cha Kongresi kinaongozwa na kamati ya chumba cha wateule, ila tu uspika wa mikutano ndio unafanyika kwa duru kati ya maprezidenti wa vyumba vyote viwili.

Kongresi pia ina haki ya kutunga kawaida yake ya ndani.
Kabla itumikishwe, kawaida hii itapelekwa na spika wa Kongresi mbele ya Korti Kuu ya Katiba kwa kuchungua usambamba wake na katiba. Korti Kuu inatoa msimamo wake kwa mda usiozidi siku 15.

Ukizidi mda huo, kawaida hiyo itaonekana kama inakubalika.

Ama vifungo vyake vitavyoonekana kuwa kinyume na katiba vitabatilishwa na kupigwa marufuku.

Kifungo cha 121*a*

Kila chumba, kama vile kongresi, havikutane ila tu vikitimiza uwingi wa kawaida wa jumla ya memba, yaani kiasi cha zaidi ya nusu kati.

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, hatua na azimio hazichukuliwe ila kufwatana na kawaida ya ndani ya kila chumba ao ya kongresi.
Kura zinafanyika ima kwa kuitwa kwa sauti kubwa, ima kwa kuinua mkono, ima kwa kusimama wima (na wengine kubaki wanakaa), ima kwa kicheti cha siri, ao tena kwa njia nyingine ya elektroniki.

Kwa kuwafiki jumla ya sharia hutumia njia ya kuita kwa sauti kubwa.

Ama kutumia njia nyingine yoyote ya kitaalam kwa kuzidisha uaminifu wa kura, kunaruhusiwa.

Bila kuhasiri vifungo vingine vya katiba, kila chumba, kama vile kongresi, kina uwezo wa kuamuru siri ya kura kwa kukubaliana kuhusu jambo fulani.
Lakini kwa kujadili kuhusu watu, inatumiziwa tu njia ya kura ya siri.

SEHEMU YA TATU :

MAWASILIANO KATI YA WATAWALA NA WATUNGA SHARIA

Kifungo cha 122*i*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, sharia mbalimbali zinahusika hasa na kufafanua kanuni na mipango kuhusu :

1. Haki za raia na zamini ya msingi wanayopewa wananchi kwa kufaulu na huru zao;
2. kawaida ya machaguzi;
3. matumizi ya mali ya serikali;
4. mapashwa ya raia juu ya nafsi na mali zao kwa ulinzi wa taifa;
5. uraia, hali na uwezo wa watu, mipango ya jamaa na vizazi, mirasi na mengine;
6. ufafanuzi wa hatia mbalimbali na azabu zinazostahili, taratibu za kuazibu mahasi, mpango na mwendo wa mahakama, uendeshaji wa vituo vya uamzi, hazi ya majaji, jisimu ya baraza kuu la uamzi;
7. mpango wa kikundi cha mawakili na wakala mbele ya vituo vya uamzi;
8. biashara, haki ya utajiri na uwenyeji, mapashwa ya kiraia na ya kibiashara;
9. kufuta hatia na kuwavua hifazi wafanya mahasi wa nchi nyingine;
10. ushuru, kodi na viwango vyake, mipango ya kuchapisha mapesa;
11. mikopo na madeni ya serikali;

12. jisimu ya watumishi wa serikali na hao wa vyuo vya juu na wa utafiti;
13. jeshi, polisi na idara za upelelezi;
14. haki ya kazi na huduma za jamii;
15. mipango jumla ya ulinzi na ya polisi, mipango ya kuajiri askari jeshi na askari polisi, kupanda cheo, haki na mapashwa ya askari na polisi.

Kifungo cha 123*u*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, sharia mbalimbali zinabainisha misingi maalumu kwa yanayohusu :

a. kujimiliki kwa majimbo na maeneo mengine ya ardhi inayojitawala, mipaka ya mamlaka yao na mapato yao;
b. kuunda mashirika, idara na taasisi za serikali;
c. ardhi, madini, misitu na majumba;
d. makundi ya kusaidiana na akiba;
e. masomo na afya;
f. mipango ya gereza;
g. mfumo wa vyama vingi vya siasa na mashirika ya utetezi wa wafanya kazi;
h. haki ya mgomo;
i. mpango wa mitambo ya habari;
j. utafiti wa sayansi na teknolojia;
k. makundi ya mawasiliano;
l. ufundi na utamaduni;
m. michezo na maburudiko;

n. mlimo, ufugo, uvuvi na mlimo wa kunyunyuzia maji;
o. kinga ya mazingira na utalii;
p. kinga ya makundi ya wazalili.

Kifungo cha 124*e*

Sharia zote zinazopewa na katiba sifa ya sharia maalumu ya uongozo haziwafikiwe ao kurekebishwa ila zikikusanya kura ya uwingi wa kawaida (zaidi ya nusu kati) ya jumla ya memba wa chumba kinachohusika, pamoja na kuheshimu masharti haya :

a. Pendekezo la sharia halijadiliwe na kupigiwa kura kunako chumba kilichohusishwa cha kwanza ila unapomalizika mda wa siku 15 tangu ilipelekwa mbele ya serikali (kwa kupata maoni yake);
b. Taratibu ya kifungo cha 132 inahusishwa.
   Bali kwa ukosefu wa maafikiano kati ya vyumba viwili sharia haiwezi kuwafikiwa kwa mwisho na chumba cha wateule, ila ikikusanya uwingi wa sauti kufikia kiasi cha zaidi ya nusu kati ya jumla ya memba wa chumba cha wateule.
c. Sharia zisiiziniwe na Rais ila baada ya kusahihishwa na Korti Kuu ya Katiba kwa mda usiozidi siku 15 baada ya kupelekwa na Rais wa jamhuri.

Kifungo cha 125*o*

Ikiwa kama serikali inahimiza pendekezo fulani ya sharia kuwa ya haraka, inajadiliwa basi kwa njia ya haraka na kamisheni maalumu kwa niaba ya chumba kinachohusika kufwatana na kawaida yake ya ndani.

Ama kuhusu miswada na pendekezo za sharia kuhusu marekebisho ya katiba ao mabadiliko ya sharia maalumu ya uongozo ao tena pendekezo za sharia za kuwazifisha kama inavoagizwa na kifungo cha 129, zinapashwa tu kufwata taratibu za kawaida

Kifungo cha 126*a*

Sharia za mali zinafafanua harakati za mapato na matumizi ya serikali.

Chumba cha wateule na hicho cha seneti vinawafiki sharia za mali kufwatana na masharti inayobainishwa na sharia maalumu ya uongozi inayozungumziwa kunako kifungo cha 124 cha katiba.

Sharia ya mali ya mwaka ambayo inahusika pia na bajeti, inapelekwa na serikali kwenyi Bunge tarehe 15 septemba ya kila mwaka, ikiwa nyuma zaidi.

Kuzaa ao kubadilisha shughuli fulani kunako idara ya serikali hakuwezi kufanyika bila ya kutezama matarajio ya sharia za mali.

Ikiwa kama pendekezo ya sharia ya mali iliyopelekwa mbele ya Bunge kwa kuheshimu mda, inachelewa kuwafikiwa kabla uanze mwaka wa matumizi, anapewa uwezo Rais wa Jamhuri, kwa pendekezo la serikali lililojadiliwa na baraza la mawaziri, kuruhusu kuitumikisha, ikipewa nafasi marekebesho mbalimbali iliyokubaliwa na kile kile chumba cha Bunge.

Ama kama pendekezo ya sharia ya mali inachelewa kupelekwa kwa kuizinishwa na Rais wa Jamhuri kabla uanze mwaka wa matumizi, serikali itakitaka chumba cha wateule kuruhusu kufungua mifuko ya matumizi ya mda.

Ama tena ikifikia siku 15 za mwisho wa kutandua kikao cha bajeti bila ya serikali kupeleka pendekezo ya bajeti mbele ya Bunge, serikali inapewa sifa ya kujiuzulu.

Na kama Chumba cha wateule na seneti havifikie hadi siku 15 kutoa rai yao kuhusu maombi ya ufunguzi wa mifuko ya matumizi ya mda, Rais wa Jamhuri ataruhusu kuitumikisha mipango iliyomo ndani ya pendekezo iliyotumwa mbele ya Bunge, kwa pendekezo la serikali iliyojadiliwa na baraza ya mawaziri.

Ikiwa kama, kufwatana na harakati inayopangwa hapa juu, itafikia tarehe mosi ya mwezi februari wa mwaka wa matumizi bila ya kutumikishwa sharia ya mali ya mwaka, kwa pendekezo ya serikali inayojadiliwa na baraza la mawaziri,

Rais wa Jamhuri ataruhusu itumikishwe pendekezo ya sharia ya mali kwa kufwatia marebisho iliyokubaliwa na kila kile chumba cha bunge.

Kifungo cha 127*a*

Haipokelewi madai yoyote ya kubadilisha pendekezo la sharia ya mali ikiwa kama italeta hasara ya kupunguza mapato ao ya kuzidisha gharama, ila tu kama itasindikizwa na fikara muhimu ya kulipiza.

Kifungo cha 128*e*

Mambo mengine ambayo haihusike na sharia inapewa tu nguvu ya ukanuni.

Hati zote za nguvu ya sharia kuhusiana na mambo haya, yanaweza kubadilishwa kwa dikrii, ikiwa kama kwa maombi ya serikali, Korti Kuu ya Katiba itaamuwa kwamba kweli ina hali tu ya kutungiwa kawaida, kuhusiana na sehemu ya kwanza ya kifungo hichi.

Kifungo cha 129*a*

Kwa kuhimiza sera yake ya kazi, serikali inaweza kukitaka chumba cha wateule au seneti ruhusa ya kuchukua amri-sharia kazaa kwa mda unaobainishwa na

kuhusu mambo bainifu ambayo kwa kawaida inahusika na nguvu ya sharia.

Amri-sharia hizo zinajadiliwa kunako baraza la mawaziri na zinatoa uwezo wake pale tu zinatangazwa na kumalizika nguvu ikiwa kama pendekezo ya sharia ya kuzipa sahihi haikufikishwa Bungeni kabla umalizike mda uliopangwa na sharia ya kuwazifisha.

Ama tena ukamalizika mda unaotajwa kunako sehemu ya kwanza ya kifungo hichi bila ya Bunge kuipa sahihi, amri-sharia hizo zinaacha zenyewe kutoa uwezo wake.

Amri-sharia zilizojadiliwa kunako baraza la mawaziri na baadae zikapewa sahihi na Bunge hazibadilishwe ila kwa sharia maalumu.

Amri-sharia zinamalizika uwezo wake ikiwa zitapigwa marufuku pendekezo za sharia za kuzipa sahihi.

Kifungo cha 130*i*

Fikara ya muswada wa sharia ni juu ya serikali na kila mteule ao kila mwanaseneti.

Pendekezo za sharia zinazowafikiwa na serikali baada ya kujadiliwa na baraza la mawaziri, zinapelekwa mbele ya kamati ya uongozi ya kimoja kati ya vyumba viwili vya bunge.

Lakini, kuhusu sharia ya mali, inadaiwa kabisa pendekezo ipelekwe mbele ya kamati ya uongozi wa chumba cha wateule kwa mda unaobainishwa na kifungo cha 126.

Kabla ianze harakati ya kujadili na kuwafiki, miswada ya sharia inajulishwa kwa serikali ambayo, kwa mda usiozidi siku 15, itatuma maoni yake mbele ya kamati ya uongozi wa kimoja kati ya vyumba viwili vya Bunge.
Ikizidi siku 15, miswada itaanza kujadiliwa.

Kifungo cha 131*a*

Memba wa serikali wana fursa ya kuhuzuria mikutano ya chumba cha wateule na hiyo ya seneti, hata ya kamisheni zao.

Ama kama wakaitishwa, inakuwa kwao ni mkazo kuhuzuria mikutano ya chumba cha wateule na hiyo ya seneti, kuzungumza na kuwapa wabunge mafasirio wanayoitaka kuhusu kazi za wizara zao.

Kifungo cha 132*i*

Kunako chumba cha kwanza kilichohusishwa, mabishano ya pendekezo za sharia inahusu hasa muswada jinsi ulivopelekwa na serikali.

Chumba kitachopelekewa pendekezo iliyokwishajadiliwa na chumba kingine hakitatizama tena muswada kwa sura yake ya asili, ila pendekezo katika sura itakayofika kwake.

Kifungo cha 133*u*

Memba wa serikali wanao wasaa wa kutoa maoni yao ya kubadili pendekezo linalojadiliwa bila ya kushiriki kwa kura.

Kifungo cha 134*e*

Pendekezo za sharia na maoni ya kuzibadilisha inayotolewa na memba wa chumba cha wateule ao wa seneti, haina nafasi ikiwa kama ikikubaliwa inaweza kuleta kinyume cha kupunguza mapato ao kuzidisha gharama za serikali, isipokuwa kama itasindikizwa na fikara maalumu ya kuzaa mapato ya kuhudumia gharama hizo.

Kifungo cha 135*o*

Kila pendekezo ya sharia inapitiwa na vyumba vyote viwili vya Bunge, hichi baada ya kile, kwa jinsi vifikie kuwafiki sharia kwa sura moja.

Na kama, kufwatana na hitilafu baina yao, pendekezo halikufikia kukubaliwa baada ya kupitiwa na kila chumba, kamati za uongozi za vyumba vyote viwili zitaunda kamisheni

ya pamoja inayokusanya memba wa vyumba vyote viwili kwa idadi ya sawa kwa sawa, kwa lengo la kutoa muswada wa maafikiano kuhusu sehemu zinazoleta matatizo.

Muswada wa kamisheni ya pamoja utapelekwa mbele ya vyumba vyote viwili kwa kusahihishwa.

Ama kama kwa upande wake kamisheni ya pamoja haikubaliane kwa kutoa fikara moja, ima muswada uliotolewa na kamisheni ya pamoja haukubaliwi kama inavyoagizwa hapa juu, basi ni juu yake chumba cha wateule kuchukua jukumu yake na kutafakari peke yake.

Hapo chumba cha wateule kina hiari ya kuchukua maandishi ya kamisheni ya pamoja, ao kurudilia pendekezo kilichokubali hapo mbele na kuchomeka, ikiwezekana, mabadiliko fulani fulani iliyopendekezwa na seneti.

Kifungo cha 136*a*

Siku sita(6) tu baada ya kuwafikiwa, sharia inatumwa mbele ya Rais wa Jamhuri kwa kuiziniwa. Waziri Mkuu pia anapelekewa nakala.

Kifungo cha 137*a*

Kwa kipindi cha siku 15 tangu kutumiwa sharia, Rais wa Jamhuri anaweza kukidai chumba cha wateule ao seneti

kurudilia vipya mjadala wa sharia yote nzima ao kuhusu vifungo vyake kazaa. Haukataliwe mjadala huu mpya.

Ama pendekezo inayopitiwa mara ya pili, inawafikiwa na chumba cha wateule ao na seneti katika hali yake ile ile ya mbele ao kwa kubadilishwa sehemu fulani fulani kwa kura ya uwingi wa kawaida, yaani zaidi ya nusu kati, wa jumla ya memba wa chumba kihusikacho.

Kifungo cha 138*e*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, njia kwa vyumba vya Bunge kupata maelezo na mafasirio wanayoitaka kwa serikali, mashirika ya serikali, idara na taasisi za serikali, ni :

a. swali la bunge, la kauli ama la maandishi, likifwatiwa na mjadala ao laa, na lisilopigiwa kura;
b. swali kuhusu matokeo ya sasa (hali ya sasa);
c. masambo ama kudai mafasirio ya pale kwa pale;
d. Tume la uchunguzi;
e. Ukaguzi wa tume fulani.

Hii ndio mipango ya uchunguzi ambayo inaendeshwa kufwatana na masharti inayobainishwa na kawaida ya ndani ya kila chumba na kufikia, saa zingine, kwa muswada wa lawama zidi ya serikali nzima ao muswada wa tuhuma zidi ya memba fulani wa serikali kwa mipango ya vifungo vya 146 na 147 vya katiba hii.

<u>Kifungo cha 139*a*</u>

Korti Kuu ya Katiba inaweza kupelekewa madai ya kuitaka isikubalishe sharia fulani kwa kutoafikiana na mipango ya katiba. Madai haya yanaweza kutoka :

- kwa Rais wa Jamhuri, kwa mda usiozidi siku 15 tangu amepelekewa sharia kama ilivowafikiwa na chumba fulani cha bunge;
- kwa serikali, kwa mda usiozidi siku 15 tangu imetumiwa nakala ya sharia kama ilivyowafikiwa na chumba fulani cha Bunge;
- kikundi cha wateule wa taifa ao cha wanaseneti kwa idadi isiyopunguwa kikumi kimoja cha jumla ya memba wa chumba chao, kwa mda usiozidi siku 15 tangu kuwafikiwa sharia na chumba chao.

Sharia hiyo haiizinishwe ila ikikubaliwa kuafikiana na katiba kwa mujibu wa hukumu ya Korti Kuu ya Katiba ambayo inalazimishwa kutoa msimamo wake kwa mda usiozidi siku 15 tangu kupelekewa madai.

Ukizidi mda huo, sharia inapewa sifa ya kuwa sawa.

<u>Kifungo cha 140*i*</u>

Rais wa Jamhuri anaizinisha sharia kwa kipindi cha siku 15 tangu aitumiwe na baada ya kumalizika mda unaozungumziwa kunako vifungo vya 136 na 137 vya katiba.

Kwa kukosa kuizinishwa na Rais wa jamhuri kwa vipindi vinavyobainishwa na katiba, sharia inajiizinisha yenyewe kisharia.

<u>Kifungo cha 141*a*</u>

Sharia zote zinapigwa muhuri wa serikali na kutangazwa kunako gazeti ya serikali.

<u>Kifungo cha 142*i*</u>

Sharia yoyote inaanza kutoa nguvu zake siku salasini (30) baada ya kutangazwa kwake kunako gazeti ya serikali, isipokuwa kama yenyewe imepanga mengine.

<u>Kifungo cha 143*u*</u>

Kwa mujibu wa kifungo cha 86 cha katiba, Rais wa jamhuri anaamuru vita kwa makubaliano na baraza la mawaziri, baada ya kupata maoni ya baraza kuu la ulinzi na kibali cha vyumba vyote viwili vya Bunge.

Anaifahamisha taifa nzima kwa njia ya hutuba.

Sharia maalumu inabainisha haki na mapashwa ya wananchi wakati wa vita ama wakati inavamiwa sehemu fulani ya nchi na vikosi kutoka njee.

Kifungo cha 144*e*

Kwa mujibu wa kifungo cha 85 cha katiba hii, Rais wa Jamhuri ndiye anatangaza hali ya wasiwasi na hali ya zarura.

Papo hapo, chumba cha wateule na seneti vinakutana. Na kama vilikuwa katika livu, kitaitishwa kikao cha zarura kufwatana na maagizo ya kifungo cha 114 cha katiba hii.

Hali ya wasiwasi ao ya zarura inaikabili sehemu ao eneo nzima ya Jamhuri kwa mda usiozidi siku salasini (30).

Amri inayotangaza hali ya wasiwasi ao ya zarura inamalizika nguvu yake hapo tu utamalizika mda unaobainishwa kunako sehemu ya tatu ya kifungo hichi, isipokuwa ikiruhusiwa na chumba cha wateule pamoja na seneti kuiongeza kwa vipindi vya kufwatana vya siku 15, kwa maombi ya Rais wa jamhuri, baada ya makubaliano na baraza la mawaziri.

Kifungo cha 145*o*

Wakati inatangazwa hali ya wasiwasi, Rais wa Jamhuri anachukua, kwa amri zinazojadiliwa na baraza la mawaziri, hatua zinazostahili kuhusiana na hali ya mambo.

Amri hizo zinatumwa, pale tu zitasainiwa, mbele ya Korti Kuu ya Katiba, itayotafakari bila kuchelewa kama haziende kinyume na katiba hii.

Kifungo cha 146*a*

Baada ya kujadiliana kunako baraza la mawaziri, Waziri Mkuu anaweza kuwakilisha serikali yake mbele ya chumba cha wateule kwa kuzungumzia sera yake, siasa ya taifa ao kukubalisha maandishi fulani.

Chumba cha wateule, kinaishutumu serikali nzima ao memba moja wa serikali kwa njia ya muswada wa lawama ao muswada wa tuhuma.

Muswada wa lawama zidi ya serikali, haupokelewi ila ukikusanya saini ya zaidi ya robo ya memba wa chumba cha wateule.

Muswada wa tuhuma zidi ya memba wa serikali haupokelewi ila ukikusanya saini ya zaidi ya kikumi kimoja cha jumla ya memba wa chumba cha wateule.

Mabishano na kura juu ya miswada hiyo inaanza masaa arubaini na nane (48) baada ya kupokelewa kwa miswada. Hapo inahisabiwa tu kura ya kuikubali miswada ambayo, kwa kawaida, inawafikiwa kwa sauti ya uwingi wa kawaida (zaidi ya nusu kati) ya jumla ya memba wa chumba cha wateule.
Na kama muswada unapigwa marufuku, waliousaini hawawezi tena kupendekeza muswada mwengine kwa kipindi cha kikao hicho.

Sera ya serikali, tangazo ya siasa ya taifa ao maandishi fulani kama ilivyotajika kunako sehemu ya kwanza ya kipindi hichi, inapata sifa ya kukubalika, isipokuwa kama unakubaliwa muswada fulani kufwatana na masharti iliyopangwa kunako sehemu ya pili na ya tatu ya kifungo hichi

Waziri Mkuu ana fursa ya kuitaka seneti kuikubali tangazo yake ya siasa ya taifa.

Kifungo cha 147*a*

Pale tu muswada wa lawama utawafikiwa na chumba cha wateule, serikali itakuwa na sifa ya kujiuzulu.

Kwa hiyo, Waziri Mkuu anahusika na kupeleka mbele ya Rais wa Jamhuri hati ya kuuzulu serikali yake kwa mda wa masaa 24 inayofwatia kuwafikiwa muswada wa lawama.

Vivo hivyo, pale tu muswada wa tuhuma zidi ya memba wa serikali utawafikiwa na chumba cha wateule, huyo atakuwa na sifa ya kujiuzulu.

Kifungo cha 148*e*

Ikitukia mivutano ya kudumu kati ya serikali na chumba cha wateule, Rais wa Jamhuri anao uwezo, baada ya kuhojiana na Waziri Mkuu na maprezidenti wa vyumba vyote viwili vya Bunge, wa kukivunja Chumba Cha Wateule.

Chumba cha wateule hakiwezi kuvunjwa kwa kipindi cha mwaka mmoja unaofwatia uchaguzi, ao wakati inatangazwa hali ya wasiwasi ao ya zarura, ao inapoamurishwa vita, ao tena wakati nchi inatawaliwa na Rais wa mda.

Kikivunjwa Chumba cha wateule, Tume Huru ya Taifa inayohusika na uchaguzi inawaitisha raia kwa kuchagua wateule wengine kwa kipindi cha siku sitini (60) inayofwatia kutangazwa amri ya Rais inayovunja chumba cha mbele.

Zitaahirishwa tarehe ya kufungwa vikao vya kawaida ama vya zarura kwa kuacha iwezekanavyo wasaa wa kutumizia mipango ya kifungo cha 144.

SEHEMU YA NNE : UWEZO WA KUAMUA SHARIA

## FUNGO LA KWANZA : MIPANGO YA JUMLA

### Kifungo cha 149*a*

Vyumba vya uamzi vinashikilia uhuru kamili zidi ya watunga sharia na viongozi watawala.

Ni juu ya Korti na mahakama, ambayo inaundwa na Korti Kuu ya Katiba, Halmashauri ya Serikali, Mahakama Kuu, Korti Kuu ya kijeshi, korti na mahakama ya kiraia na ya kijeshi pia na vituo vya wakata mashataka wa serikali vinavyoungwa kunako vyumba hivyo, uwezo wa kuamua sharia.

Haki inaamuliwa katika eneo nzima ya nchi kwa niaba ya umma.

Hukumu na maamzi yote, pia na amri za korti na mahakama zinatumikishwa kwa niaba ya Rais wa Jamhuri.

Inaharamishwa kabisa kuunda mahakama mengine ya kipekee ama ya zarura kwa jina lolote lile.

Vyumba vya uamzi vina hazina yake ya kipekee ambayo inapangwa na baraza kuu la uamzi na kutumwa mbele ya serikali kwa kupewa nafasi ndani ya bajeti ya jumla ya serikali. Prezidenti wa kwanza wa Mahakama Kuu ndiye muamrishaji wa matumizi ya hazina akisaidiwa na Katibu Mripoti wa baraza kuu ya uamzi.

Kifungo cha 150*i*

Vyumba vya uamzi ndivyo vinazamini huru za kibinafsi na haki za msingi za wananchi.

Katika kuendesha kazi zao, majaji hawana juu yao hukumu nyingine yoyote ila tu hiyo ya sharia.

Sharia maalumu ya uongozi inabainisha jisimu ya majaji na mahakimu.

Maafisa wa sharia hawahamishwe ila kwa kuteuliwa kwa cheo kingine ao kwa maombi yao wenyewe ao tena kwa hatua ya mabadiliko ya jumla inayokusudiwa na baraza kuu la uamzi kwa kisa maalumu.

Kifungo cha 151*a*

Viongozi watawala hawana ruhusa ya kuwapa majaji agizo lolote katika kuendesha kazi zao, wala uwezo wa kuamua mizozano kati ya watu, wala kutilia pingamizi kesi yoyote, wala kukataa itumikishwe hukumu ya jaji.

Pia, watunga sharia hawana ruhusa ya kutafakari kuhusu mivutano ya kisharia, wala kubadilisha hukumu ya jaji ao kupinga kutumikishwa kwake.

Sharia yoyote ambayo itaoonekana kwamba ukomo wake ni kuleta suluhu kuhusiana na kesi inayoendeshwa mbele ya vituo vya uamzi, haina nafasi wala nguvu yoyote.

Kifungo cha 152*i*

Baraza Kuu ya uamzi ndio chumba kinachomiliki vyumba vya uamzi.

Baraza Kuu ya uamzi inaundwa na :

- Prezidenti wa Korti Kuu ya Katiba
- Mkata mashtaka Mkuu kunako Korti Kuu ya Katiba
- Prezidenti wa kwanza wa Mahakama Kuu
- Mkata mashtaka mkuu kunako Mahakama Kuu
- Prezidenti wa kwanza wa Halmashauri ya serikali;
- Mkata mashtaka mkuu kunako Halmashauri Kuu ya serikali
- Prezidenti wa kwanza wa Korti Kuu ya kijeshi
- Mkata mashtaka mkuu kunako Korti Kuu ya kijeshi
- Maprezidenti wa kwanza wa korti kuu za majimbo
- Wakata mashtaka wakuu kunako korti kuu za majimbo
- Maprezidenti wa kwanza wa Korti za uongozi za majimbo
- Wakata mashtaka wakuu kunako korti za uongozi za majimbo
- Maprezidenti wa kwanza wa korti za kijeshi majimboni
- Wakata mashtaka wakuu wa kijeshi majimboni
- Mahakimu wawili kwa kila eneo la korti kuu ya jimbo wanaochaguliwa na jumla ya wenzi wao kwa kipindi cha miaka mitatu

- Wakata mashtaka wawili kwa kila eneo la korti kuu ya jimbo wanaochaguliwa na wenzi wao kwa kipindi cha miaka mitatu
- Hakimu mmoja kwa eneo ya korti ya kijeshi
- Mkata mashtaka mmoja kwa eneo ya korti ya kijeshi.

Baraza kuu ya uamzi inafanya mapendekezo ya kuteuliwa, ya kupandishwa daraja na ya kuachishwa kazi mahakimu.
Inao uwezo wa azabu zidi ya mahakimu.
Inatoa maoni yake kuhusu maombi ya msamaha.

Sharia maalumu ya uongozi inazihirisha mpango wa uendeshaji wa baraza Kuu la uamzi.

FUNGO LA PILI : KUHUSU VITUO VYA JUMUIYA YA UAMZI

Kifungo cha 153*u*

Inaundwa hivi sasa jumuiya ya vituo vya uamzi ambayo inakusanya korti na mahakama ya kisharia chini ya uchunguzi wa Mahakama Kuu.

Bila kuhasiri mamlaka yake mengine inayobainishwa na katiba hii ao na sharia mbalimbali za jamhuri, Mahakama Kuu inapokea rufaa zidi ya hukumu na maamzi iliyotolewa kwa duru ya kwanza na Korti na Mahakama ya kiraia na ya kijeshi.

Kwa mujibu wa masharti inayobainishwa na katiba na sharia mbalimbali za Jamhuri, Mahakama Kuu inapokea kwa duru ya kwanza na ya mwisho, shutuma za hatia zilizofanywa na :

- Memba wa chumba cha wateule na wa seneti;
- Memba wa Korti Kuu ya Katiba;
- Majaji wa Mahakama Kuu na Wakata mashtaka wa serikali kunako mahakama kuu;
- Memba wa halmashauri Kuu ya serikali na wakata mashtaka wa serikali kunako halmashauri kuu ya serikali;
- Memba wa Korti Kuu ya hisabu na wakata mashtaka wa serikali kunako korti kuu ya hisabu;
- Maprezidenti wa kwanza wa korti kuu za majimbo na wakata mashtaka wakuu kunako korti kuu za majimbo;
- Maprezidenti wa kwanza wa korti za uongozi za majimbo na wakata mashtaka wakuu kunako korti hizo;
- Maliwali wa majimbo na makamu wao pamoja na mawaziri wa majimbo;
- Maprezidenti wa vyumba vya wateule vya majimbo.

Korti na mahakama, ya kiraia kama vile ya kijeshi, inatekeleza mikataba ya kimataifa iliyoratibiwa nchini, sharia mbalimbali, hati za kikawaida ambazo zinaafikiana na sharia, na desturi ya kyenyeji ikiwa haiende kinyume na mpango wa usalama na mila mizuri.

Mpangilio, uendeshaji na mamlaka ya vituo vya jumuiya ya uamzi vinabainishwa na sharia maalumu ya uongozi.

FUNGO LA TATU : VITUO VYA JUMUIYA YA UONGOZI

Kifungo cha 154*e*

Inaundwa nchini jumuiya ya vituo vya uongozi ikijumuisha Halmashauri Kuu ya serikali na korti na mahakama ya uongozi.

Kifungo cha 155*o*

Bila kuhasiri mamlaka yake mengine kama inavyopangwa na katiba hii ao na sharia, Halmashauri Kuu ya serikali inapokea, kwa duru ya kwanza na ya mwisho, malalamiko kuhusu uhalifu wa sharia zidi ya hati, kanuni na hatua za viongozi watawala wa taifa.

Inapokea pia rufaa kuhusu maamzi iliyotolewa na korti za uongozi za majimbo.

Inapokea tena, ikiwa hakikuweko kituo kinachohusika, maombi ya faini kuhusu mazara ya kipekee, ya hali ao ya mali, iliyotukia kutokana na hatua zilizochukuliwa na wakuu viongozi wa taifa.

Inaamua kwa uadilifu mkubwa, ikitarajia faida ya umma na ya binafsi.
Mpango, uendeshaji na mamlaka ya vituo vya uongozi vinabainishwa na sharia maalumu.

## FUNGO LA NNE : VITUO VYA KIJESHI

### Kifungo cha 156*a*

Vituo vya kijeshi vinapokea hatia zote zinazofanyizwa na memba wa jeshi na wa polisi.

Wakati wa vita ao ikitangazwa hali ya wasiwasi ama ya zarura, Rais wa Jamhuri, kwa hatua inayojadiliwa na baraza la mawaziri, anaweza kuzuwiya, katika eneo nzima ao sehemu fulani ya Jamhuri, kwa mda fulani na kuhusu hatia zinazobainishwa, mamlaka ya korti na mahakama ya kiraia na kuviachia tu nafasi vituo vya kijeshi.

Lakini, haki ya rufaa haizuwiliwi.

Kawaida na mamlaka, mipangilio na uendeshaji wa vituo vya kijeshi, zinabainishwa na sharia maalumu.

## SEHEMU YA TANO : KUHUSU KORTI KUU YA KATIBA

### Kifungo cha 157*a*

Inaundwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Korti Kuu ya Katiba.

### Kifungo cha 158*e*

Korti Kuu ya Katiba ina memba tisa (9) wanaoteuliwa na Rais wa Jamhuri, wa tatu kwa hiari yake mwenyewe, watatu kwa pendekezo ya Bunge katika kikao cha Kongresi, na watatu kwa pendekezo la Baraza Kuu la uamzi.

Sulusi mbili (2/3) ya memba wa Korti Kuu ya Katiba wanapashwa kuwa wataalamu wa mambo ya sharia kutoka kunako vyumba vya uamzi, mashirika ya mawakili ao vyuo vikuu.

Mda wa memba wa Korti Kuu ya Katiba ni wa miaka tisa isiyorudiliwa tena.

Kila mwaka inabadilishwa sulusi moja (1/3) ya memba wa Korti Kuu ya Katiba.

Hapo, kwa kila mabadiliko, atapigiwa kura memba moja wa kila kikundi (anayestahili kuachishwa nafasi yake).

Prezidenti wa Korti Kuu ya Katiba anachaguliwa na wenzi wake kwa mda wa miaka mitatu inayoweza kurudiliwa mara moja tu.

Anatawazishwa na amri ya Rais wa Jamhuri.

Kifungo cha 159*a*

Hawezi mtu yeyote kuteuliwa memba wa Korti Kuu ya Katiba,

a. kama si mkongomani;
b. kama hana uzoefu wa miaka 15 katika mambo ya sharia na ya siasa.

Kifungo cha 160*i*

Korti Kuu ya Katiba inapewa uwezo wa kuchungua usambamba na katiba wa sharia ao wa hati zilizopewa nguvu ya sharia.

Sharia maalumu za uongozi, kabla ziizinishwe, na kawaida ya ndani ya vyumba vya Bunge na Kongresi, ya Tume Huru ya taifa inayohusika na uchaguzi na ya Halmashauri ya mitambo ya habari na mawasiliano, kabla zitumikishwe, zinapashwa kupelekwa mbele ya Korti Kuu ya Katiba ambayo inatoa maoni yake kuhusu usambamba wake na katiba.

Kwa nia hiyo hiyo ya kuchungua usambamba na katiba, sharia zinaweza kupelekwa mbele ya Korti Kuu ya Katiba kwa fikara ya Rais wa Jamhuri, ya Waziri Mkuu, ya Prezidenti wa chumba cha wateule, ya Prezidenti wa seneti ao ya kikumi kimoja cha wateule ao cha wanaseneti.

Korti Kuu ya Katiba inatafakari kwa mda wa mwezi moja. Lakini, kwa maombi ya serikali ama kukitakika haraka, mda huo unafupishwa kwa siku nane.

Kifungo cha 161*a*

Korti Kuu ya Katiba inaweza kupokea maombi ya kusherehisha katiba kwa mahitaji kutoka kwa Rais wa

Jamhuri, kwenyi serikali, kwa Prezidenti wa seneti, kwa Prezidenti wa chumba cha wateule, kwa kikumi kimoja cha memba wa chumba kimoja cha bunge, kwa maliwali wa majimbo na kwa maprezidenti wa bunge za majimbo.

Inaamua pia hitilafu za machaguzi ya Rais na ya wabunge, na za kura ya maoni.

Inapokea mizozo ya mamlaka kati ya viongozi watawala na watunga sharia, na kati ya serikali kuu na majimbo.

Inapokea pia rufaa zidi ya hukumu na maamzi iliyotolewa na mahakama kuu na halmashauri ya serikali kuhusu tu uwezo kwa kile ao hichi kituo kuhusishwa na jambo fulani.
Rufaa hii haipokelewi ila tu ilipokuwa ikiendeshwa kesi imependekezwa neno la kupinga ama kushakia uwezo wa mahakama kuu ao halmashauri ya serikali.

Namna ya kukata rufaa na maombi inayotajwa kunako sehemu za hapa juu, inafafanuliwa na sharia.

Kifungo cha 162*i*

Korti Kuu ya Katiba ndio kituo cha kuamua shaka ya ukatiba iliyopendekezwa mbele ya kituo fulani ao na kituo kazaa.
Mtu yeyote ana haki ya kupeleka madai yake mbele ya Korti Kuu ya Katiba kuhusu shaka ya ukatiba wa hati ya kisharia ama ya kawaida fulani.

Anayo pia haki ya kuipelekea Korti Kuu ya Katiba madai kuhusu shaka ya ukatiba anayoipendekeza katika kesi inayomhusu mbele ya kituo fulani cha uamzi.

Kituo hichi kitasimamisha kesi na kuielekea pale kwa pale Korti Kuu ya Katiba.

Kifungo cha 163*u*

Korti Kuu ya Katiba ndio kituo kinacho uwezo wa azabu zidi ya Rais wa jamhuri na Waziri Mkuu, kwa mujibu wa masharti inayoagizwa na katiba.

Kifungo cha 164*e*

Korti Kuu ya Katiba ndio kituo kinachopewa uwezo wa azabu zidi ya Rais wa jamhuri na Waziri Mkuu kwa hatia za kisiasa kuhusu usaliti, kuikosea heshima Bunge, mazara zidi ya heshima na uadilifu na shutuma za kudokezwa pia na hatia mbalimbali za kawaida walizotenda kipindi ao kwa mujibu wa kipindi cha utawalo wao.

Ina pia uwezo wa kuwasambisha waliosharikiana nao ao waliohusika kwa pamoja nao.

Kifungo cha 165*o*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, hatia ya usaliti inapatikana wakati Rais wa Jamhuri anahalifu kusudi katiba ao wakati yeye, ao Waziri Mkuu wanasibitishwa kuwa waanzishaji, washiriki ao wahusikao na njama ya kuvunja haki za wanaadamu ao ya kupana sehemu ya ardhi ya nchi.
Inapatikana hatia ya kuzuru heshima ao uadilifu wakati mwendo binafsi wa Rais wa jamhuri ao wa Waziri Mkuu unaenda kinyume na mila mizuri ama wakisibitishwa kuwa waanzishaji, washiriki ao wahusikao katika njama ya kuiba mali ya serikali, ya kula rushwa ao ya kutajirika kwa njia isiyokuwa halali.

Inapatikana zidi ya Rais wa Jamhuri ama zidi ya Waziri Mkuu hatia ya kudokezwa, wakati anafanya operesheni ya samani ya majumba ao vifaa ambavyo amepelekewa habari ya kipekee na kujipatia faida ya kibinafsi kabla habari hiyo ijulikane na watu wengine.
Hatia ya kudokezwa inakusanya pia kununua ama kuuza vidamu kutokana na taarifa ambazo hazijajulishwa kwa washirika wengine.

Inapatikana hatia ya kuikosea Bunge wakati, kwa maswali aliyopelekewa na kimoja kati ya vyumba vya Bunge kuhusu kazi na shuruli za serikali, Waziri Mkuu anakosa kurudisha majibu kwa kipindi cha siku salasini (30).

Kifungo cha 166*a*

Hatua ya kumshutumu na kumsambisha Rais wa Jamhuri ao Waziri Mkuu inaruhusiwa kwa kura ya uwingi wa sulusi mbili (2/3) ya memba wa bunge wanaounda Kongresi, kufwatana na taratibu iliyoazimishwa na kawaida ya ndani.

Hatua ya kuwashutumu na kuwasambisha memba wa serikali inaruhusiwa kwa kura ya uwingi wa kawaida, yaani zaidi ya nusu kati, ya jumla ya memba wa chumba cha wateule, kufwatana na taratibu iliyopangwa na kawaida ya ndani ya Chumba cha wateule.

Memba wa serikali anayepelekewa mbele ya Korti Kuu ya Katiba analazimishwa kujiuzulu kwa kazi yake.

Kifungo cha 167*a*

Wakakatiwa hukumu, Rais wa Jamhuri na Waziri Mkuu wanaachishwa kazi.

Tangazo la kuwaachisha kazi linatolewa na Korti Kuu ya Katiba.

Ama kwa makosa mengine wanayoifanya njee ya kazi zao, mashtaka yote zidi ya Rais wa Jamhuri na Waziri Mkuu inasimamishwa hadi kitapomalizika kipindi chao cha kazi. Vile vile mda wa kumalizika mashtaka unasimamishwa.

Kifungo cha 168*e*

Hukumu za Korti Kuu ya Katiba hazikatiwi rufaa na zinatekelezwa pale kwa pale. Ni za Kushurutisha na zinalazimishwa kwa viongozi watawala, kwa wakuu wa maeneo ya kujimiliki na wa vituo vya sharia, vya kiraia kama vile vya kijeshi, na kwa watu binafsi.

Hati yoyote itayotangazika kuwa kinyume na katiba, inabatilika yenyewe.

Kifungo cha 169*a*

Mpango na uendeshaji wa Korti Kuu ya Katiba vinafafanuliwa na Sharia maalum ya uongozi.

SEHEMU YA SITA : KUHUSU MALI YA SERIKALI

FUNGO LA KWANZA : MIPANGO YA JUMLA

Kifungo cha 170*i*

Franka ya Kongo ndio kipimo cha feza nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Inao uwezo wa ukombozi (wa kibiashara) katika eneo nzima ya nchi.

Kifungo cha 171*a*

Mali ya serikali kuu na hiyo ya majimbo inatengana mbalimbali kabisa.

Kifungo cha 172*i*

Kipindi cha matumizi ya mali kinaanza tarehe mosi yanuari na kumalizika tarehe 31 desemba.

Kifungo cha 173*u*

Hisabu jumla ya matumizi ya Jamhuri inapelekwa kila mwaka mbele ya Bunge na Korti Huu ya Hisabu ikiwa pamoja na maoni yake.

Hisabu jumla ya matumizi ya Jamhuri inakubalishwa na sharia.

Kifungo cha 174*e*

Haiwezi kupangwa kodi ila kwa njia ya sharia.
Mchango kunako gharama ya serikali ni wajibu wa kila mtu anayeishi ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Haiwezi kutiliwa kitenguzi ao kupunguziwa kiwango cha kodi ila kwa mujibu wa sharia.

Kifungo cha 175*o*

Bajeti ya mapato na matumizi ya serikali, yaani hiyo ya serikali kuu na hiyo ya majimbo, inapangwa kwa sharia kila mwaka.

Mgao wa mapato ya kitaifa inayopewa majimbo ni wa kiasi cha asili mia arubaini (40%). Kiwango hicho kinachukuliwa kuko huko.

Sharia inabainisha majina ya mapato mengine ya ndani na jinsi ya mgao wake.

## FUNGO LA PILI : KUHUSU BENKI KUU

### Kifungo cha 176*a*

Benki Kuu ya Kongo ndio taasisi maalumu ya kuchapa mapesa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kwa hiyo, Benki Kuu ya Kongo inapewa jukumu :

1. ya kulinda hazina ya serikali;
2. ya kukinga ustawi wa mapesa;
3. ya kupanga na kutumikisha siasa ya mapesa;
4. ya kuchungua jumla ya shuruli za mabenki;
5. ya kuishauri serikali kuhusu uchumi na mapesa.

Benki Kuu ya Kongo ina uhuru kamili katika kuendesha shuruli zake na mamlaka yake. Inayo ihtiari ya kujiendesha.

### Kifungo cha 177*a*

Mpango na uendeshaji wa benki Kuu ya Kongo vinabainishwa na sharia maalumu ya uongozi.

## FUNGO LA TATU : KUHUSU KORTI YA HISABU

### Kifungo cha 178*e*

Inaundwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo Korti ya Hisabu.

Korti ya hisabu ni taasisi inahusiana na chumba cha wateule.

Memba wa Korti ya Hisabu wanateuliwa, wanaachishwa kazi na kufukuzwa kazini, ikiwa lazima, na Rais wa Jamhuri kwa maoni ya Chumba cha wateule.

Memba wa Korti ya Hisabu wanapashwa kuwa na sifa ya taalima ya juu ya mambo ya mapesa, ya sharia ao ya uongozi, na uzoefu wa kazi usiopunguwa miaka 10.

### Kifungo cha 179*a*

Muundo, mpango na uendeshaji wa Korti ya Hisabu vinafafanuliwa na sharia maalumu ya uongozi.

## FUNGO LA NNE : SANDUKU LA TAIFA LA KUSAWAZISHA

### Kifungo cha 180*i*

Inaundwa nchini sanduku la taifa la kusawazisha. Sanduku hili lina nafsi yake mbele ya sharia.

Sanduku la taifa la kusawazisha linashurulikia kuhudumia miradi na sera ya vidamu vya serikali kwa lengo la kulingania mfungamano wa taifa na kusawazisha tofauti ya maendeleo kati ya majimbo na kati ya maeneo mengine ya kujimiliki.

Sanduku hili lina bajeti yake ambayo kila mwaka inatunukiwa na hazina ya serikali kwa kiasi cha asili mia kumi (10%) ya jumla ya mapato ya sifa ya kitaifa inayohusu serikali kuu.

Inawekwa chini ya uchunguzi wa serikali.

Sharia maalumu inabainisha mipangilio na uendeshaji wake.

## SEHEMU YA SABA : KUHUSU POLISI YA TAIFA NA MAJESHI

## FUNGO LA KWANZA : KUHUSU POLISI YA TAIFA

### Kifungo cha 182*i*

Polisi ya taifa ndio inahusishwa na usalama wa jumuiya, usalama wa watu na mali yao, kulinda ukimya na ukingo wa karibu wa wakuu watawala.

Kifungo cha 183*u*

Polisi ya taifa haihusike na siasa. Inatumika ajili ya taifa la Kongo. Hana ruhusa mtu yeyote kuitumizia polisi kwa faida yake binafsi.

Polisi ya taifa inaendesha shuruli zake kunako eneo nzima ya nchi, katika kuheshimu katiba hii na sharia zingine za Jamhuri.

Kifungo cha 184*e*

Polisi ya taifa inawekwa chini ya amri ya Mkuu kiongozi wa kiraia na kuwa chini ya uwezo wa wizara ya mambo ya ndani.

Kifungo cha 185*o*

Idadi ya wanapolisi kwa kila daraja na kupewa cheo cha uongozi vinapashwa, kwa kila nyakati na kwa kila jambo, kuheshimu vigezo maalumu viadilifu, vikitegemea afia ya mwili, kuelimika kwa kutosha, mwenendo mzuri na pia uwakilishi sawa kwa sawa wa majimbo.

Sharia maalumu inabainisha mpango na uongozi wa Polisi ya taifa.

FUNGO LA PILI : KUHUSU MAJESHI

Kifungo cha 187*a*

Majeshi ni mchanganyiko wa vikosi vya ardhi, vya anga, vya maji na idara mbalimbali za usaidizi wa vikosi.

Majeshi inahusishwa na kukinga ardhi na mipaka ya nchi.
Kwa mujibu wa masharti ya sharia, majeshi inaleta mchango wake katika juhudi za maendeleo ya kiuchumi, ya kijamii na ya kitamaduni, na katika ulinzi wa watu na mali yao, wakati wa amani.

Kifungo cha 188*e*

Majeshi ina sifa ya kijamhuri na inatumikia taifa nzima.
Mtu yeyote hawezi kutumizia majeshi kwa shida zake binafsi. Atashtakiwa huyo kusaliti.

Majeshi haihusike na siasa na inatiwa chini ya amri ya viongozi wa kiraia.

Kifungo cha 189*a*

Idadi ya askari kwa kila daraja na kupewa  cheo cha uongozi vinapashwa, kwa kila nyakati na kwa kila jambo, kuheshimu vigezo maalumu viadilifu, vikitegemea afya ya mwili, kuelimika kwa kutosha, mwenendo mzuri na pia uwakilishi sawa kwa sawa wa majimbo.

Kifungo cha 190*i*

Pamoja na makemeo ya kushutumiwa kwa hatia ya usaliti, hairuhusiwe mtu yeyote kupanga mafunzo ya kijeshi, ao inayohusiana na kijeshi, ao kuunda jeshi la kipekee, ao tena kuunda vikundi vya vijana wanaoshika silaha.

Kifungo cha 191*a*

Sharia maalumu inabainisha mpango na uongozi wa majeshi.

Kifungo cha 192*i*

Inaundwa halmashauri kuu ya ulinzi.

Halmashauri ya ulinzi inaongozwa na Rais wa Jamhuri akiwakilishwa na Waziri Mkuu, akikosekana ao akiwa na kizuwizi.

Mpango,muundo, mamlaka na uendeshaji wa Halmashauri Kuu ya ulinzi vinafafanuliwa na sharia maalumu.

SEHEMU YA NANE : KUHUSU IDARA ZA SERIKALI

Kifungo cha 193*u*

Idara za serikali hazihusike na siasa. Zinasimama adili wala hazipendelee upande ao mtu yeyote. Haruhusiwi mtu yeyote kutumizia idara za serikali kwa shida zake za kibinafsi.

Idara za serikali ni mchanganyiko wa jumla ya watumishi wa serikali na hao wa mitandao na taasisi nyingine inayohusika na shuruli mbalimbali za serikali.

### Kifungo cha 194*e*

Sharia maalumu inabainisha mpango na matumikio ya idara za serikali kuu, za majimbo na za maeneo inayojimiliki.

## MLANGO WA NNE
## KUHUSU MAJIMBO

### KIPINDI CHA KWANZA
### VYUMBA VYA UONGOZI WA MAJIMBO

### Kifungo cha 195*o*

Vyumba vya uongozi wa majimbo ni :

1. Bunge la jimbo;
2. Serikali ya jimbo.

Kifungo cha 196*a*

Majimbo yanaendeshwa kufwatana na misingi iliyotajwa kunako kifungo cha tatu cha katiba hii.

Mgao wa maeneo ya ndani ya jimbo unabainishwa na sharia maalumu.

Kifungo cha 197*a*

Bunge la jimbo ndio chumba cha mashauri jimboni.
Bunge la jimbo linajadili kuhusu mambo yote inayohusiana na uwezo wa jimbo na inachungua mwendo wa kazi za serikali ya jimbo na idara za serikali kwa daraja la jimbo na mitaa.

Memba wake huitwa wateule wa jimbo.

Wanachaguliwa moja kwa moja na raia kwa kura ya siri na wengine kuteuliwa kwa kipindi cha miaka mitano inayoweza kurudiliwa.

Idadi ya wateule wa jimbo wa kuteuliwa haiwezi kuzidi kikumi kimoja cha idadi jumla ya memba wa Bunge la jimbo.
Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, maagizo ya vifungo 100, 101, 102, 103, 108 na 109 inatumika, kwa kuambatanisha kinachostahili, kwenyi Bunge la jimbo.

Kifungo cha 198*e*

Serikali ya jimbo inaundwa na liwali mmoja, makamu wake mmoja na mawaziri wa jimbo.

Liwali na makamu wake wanachaguliwa na wateule wa jimbo kutoka ndani ya Bunge la jimbo ao njee ya Bunge, kwa kipindi cha miaka mitano inayoweza kurudiliwa mara moja tu. Wanatawazishwa na amri ya Rais wa jamhuri.

Mawaziri wa jimbo wanateuliwa na liwali ndani ya Bunge ao njee ya Bunge.

Mpango wa serikali ya jimbo unatizama pia uwakilishi wa jimbo nzima.

Idadi ya mawaziri wa jimbo haizidi watu kumi (10).

Kabla ya mawaziri wa jimbo kuanza kazi, liwali anapeleka mbele ya Bunge la jimbo sera ya serikali yake.

Kama sera hii inawafikiwa na uwingi wa kawaida, yaani zaidi ya nusu kati ya jumla ya memba wa Bunge la jimbo, hapo wanatawazishwa mawaziri.

Memba wa serikali ya jimbo wanaweza kuondolewa kwa pamoja ao kwa binafsi kutokana na muswada wa lawama ao wa tuhuma wa Bunge la jimbo.

Maagizo ya vifungo 146 na 147 vya katiba hii inatumika pia, kwa kuambatanisha kinachostahili, kwa mawaziri wa jimbo.

Kifungo cha 199*a*

Majimbo mawili, ama zaidi, yanaweza, kwa makubaliano, kuunda kiungo fulani cha mahojiano na uendeshaji wa siasa yao, na kuongoza kwa pamoja taasisi fulani ambazo zinatizama mambo inayohusiana na mamlaka ya majimbo.

Kifungo cha 200*i*

Inaundwa nchini Baraza la maliwali wa majimbo.

Baraza hii ina lengo ya kuleta maoni na kutoa fikara kuhusu siasa ya kuendesha, na kuhusu sharia mbalimbali zinazostahili kutungwa kwa uongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Licha ya maliwali wa majimbo, wanakutana pia katika baraza hii ya maliwali, Rais wa Jamhuri, Waziri Mkuu na waziri wa mambo ya ndani. Wanaweza pia kualikwa memba wengine wa serikali.

Baraza ya maliwali inakutana chini ya uongozi wa rais wa jamhuri.

Inakutana kwa uchache mara mbili kwa mwaka, kwa wito wa Rais wa Jamhuri.

Vikao vyake vinafanyika kwa duru ndani ya kila jimbo.

Sharia maalumu inabainisha jinsi ya kuipanga na kuiendesha baraza ya maliwali.

KIPINDI CHA PILI

KUHUSU MGAO WA MAMLAKA KATI YA SERIKALI KUU NA MAJIMBO.

Kifungo cha 201*a*

Mgao wa mamlaka kati ya serikali kuu na majimbo unabainishwa na katiba hii.

Mambo mbalimbali yanaweza kuhusika, haya na mamlaka pekee ya serikali kuu, yale na mamlaka pekee ya jimbo na mengine na mamlaka ya kuchangia serikali kuu na majimbo.

Kifungo cha 202*i*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, mambo yafwatayo yanahusu mamlaka pekee ya serikali kuu :

1. siasa ya kigeni, ikiwemo mawasiliano ya kidiplomasia na mikataba ya kimataifa;
2. kawaida ya biashara ya kimataifa;
3. uraia, hali na kanuni kuhusu wageni (wasiokuwa wakongomani);
4. kuwatoa wahasi mbele ya mahakama ya nchi nyingine, kuingia, kutoka nchini na kupana jawaza na viza;
5. usalama wa njee;
6. ulinzi wa taifa
7. polisi ya taifa;
8. utumishi wa serikali kwa ngazi ya taifa;
9. mali ya jamhuri;
10. kodi ya mapato, kodi ya mashirika na kodi ya nafsi kuhusiana na kifungo cha 174;
11. deni ya serikali;
12. mikopo kutoka njee kwa shida ya Jamhuri na majimbo;
13. mikopo ya ndani kwa shida ya Jamhuri;
14. pesa : kuchapa mapesa na samani ya sarafu;
15. kilo, vipimo na kampyuta;
16. kastamu na ushuru wa kuingiza na kutoa vifaa;
17. kawaida kuhusu mabenki na operesheni za benki na za mifuko;
18. kawaida ya mvunjo wa pesa;
19. uwenyeji wa mali ya utungaji, ya ufundi na ya uvumbuzi, na hati za uvumbuzi;
20. posta na mitambo ya mawasiliano, ikiwemo simu, redio, televisheni na vituo vya sateliti;

21. usafiri wa baharini na wa ndani : wa anga, wa reli; mabarabara na njia za mawasiliano, ya kawaida ao ya kujenga, inayounganisha majimbo ao nchi na nchi nyingine ao iliyopewa na sharia sifa ya kitaifa hata ikiwa yote nzima ndani ya jimbo fulani tu;
22. universiti na vyuo vya juu vya elimu ya kisayansi, ya kifundi ao ya kazi, vilivyoundwa na kuhudumiwa na serikali kuu, hata na serikali za majimbo kama zimepewa na sharia ya taifa sifa ya kuwa na faida ya taifa nzima;
23. kuweka mipango ya mafunzo inayohusu nchi nzima;
24. kuagiza ao kupata vifaa kwa matumizi ya Jamhuri, kwa bila kuhasiri maagizo ya kifungo cha 34;
25. kutunga sera za mlimo, misitu na za nguvu mbalimbali kwa faida ya taifa na kusimamia sera za faida ya majimbo; taasisi za mazao ya mashamba na miradi mingine ya mfano huo na kuwapanga kazini viongozi wa idara kufwatana na kawaida ya wafanya kazi wa idara za serikali; mfumo wa nguvu mbalimbali, wa mlimo, wa misitu kuhusu mawindo na uvuvi na kuhusu ulinzi wa mazingira (minyama na nyika), kudaka minyama, bizaa ya chakula kutokana na minyama na matunzo ya minyama;
26. ukingo zidi ya madhara kutokana na matumizi ya nguvu fulani ao kuambukia kwa vichembe vya kinuklea, kutokomeza kile chote kinachoweza kueneza na kusambaza vichembe vya kinuklea;
27. kukinga zidi ya mashawishi na mazara ya vikundi vya pawa za mali ya kimataifa;

28. rasilimali ya kihistoria, majumba ya athari ya historia, mashamba ya wanyama iliyopewa sifa ya kitaifa;
29. idara ya majira na usimamizi wa kitaalamu wa idara ya elimu za udongo, taswira na maji;
30. kuteuwa na kuwatuma wachunguzi wa majimbo wa mafunzo ya msingi, ya sekondari, ya kazi na ya kipekee;
31. hisabu na daftari ya watu kwa faida ya taifa nzima;
32. sera ya taifa;
33. utafiti wa sayansi na teknolojia;
34. mipango ya uongozi ya kitaifa kuhusu maendeleo ya viwanda, mabandari, viwanja vya ndege na stesheni za njia ya reli;
35. kuhudumia askari wa zamani na wajeruhi wa vita;
36. kutunga sharia kuhusu :
    a. taratibu za biashara, ikiwemo mashirika ya zamana, kuunda na kukubalisha mashirika;
    b. taratibu za azabu na kawaida ya jela;
    c. mpango na mamlaka ya vituo vya sharia na taratibu za uamzi;
    d. kawaida ya kazi huru;
    e. kawaida ya kazi, ikiwemo sharia ya mawasiliano kati ya wafanya kazi na matajiri wao, usalama wa wafanya kazi, kanuni kuhusu kinga ya jamii na huduma ya wasio na kazi;
    f. kawaida za kiuchumi, sharia kuhusu madini, mawe, mafuta, viwanda, vino vya nguvu na ulinzi wa rasilimali ya asili;
    g. kawaida kuhusu ufundi na kazi;

h. kawaida kuhusu uganga na ufundi wa tiba, chanjo za kukinga, elimu ya afya, usafi, kinga ya mama na mtoto, kawaida kuhusu kazi ya kuuza madawa, biashara za dawa, kuhusu kuingia nchini ao kukatiza nchi, kawaida za kimataifa kuhusu matibabu, kawaida ya afya ya kazi, mgao wa waganga nchini;
i. sharia za uchukuzi;
j. kawaida kuhusu utengenezaji, usahihishaji, uagizaji na usafirishaji na uuzaji wa mivuke ya kulevya;
k. kawaida kuhusu utengenezaji, uagizaji na usafirishaji wa vinywaji vya kulevya na visivyokuwa vya kulevya;
l. kawaida kuhusu utengenezaji, uagizaji, usafirishaji na ukatizaji wa vifaa vya vita;
m. kawaida kuhusu kumpa mtu uzazi kwa njia ya kitaalamu, kuhusu kupapasa taarifa juu ya elimu ya uzazi na kupandikiza viungo na nofu za mtu;
n. kawaida kuhusu wakimbizi, wanaofukuzwa na wanaohamishwa;
o. kawaida za kujiunga na kukubaliwa kunako jumuiya ya waganga na jumuiya za kazi nyingine.

Kifungo cha 203*u*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, mambo yafwatayo ndio yanahusika na mamlaka ya kuchangia kati ya serikali kuu na majimbo :

1. mipango ya kukinga na kukuza haki za wanaadamu;
2. haki za raia na za asili;

3. daftari na hisabu ya watu;
4. usalama wa ndani;
5. uongozi wa korti na mahakama, wa mahala pa kuzuwilia washutumiwa na jela za kuazibu;
6. maisha ya kitamaduni na ya michezo;
7. kupanga kodi, hususa ushuru kuhusu bizaa na vifaa fulani, kutia pande kodi zilizozungumziwa kunako kifungo cha 174;
8. utendaji wa hatua kuhusu kawaida ya wageni;
9. utafiti wa kisayansi na wa kiteknolojia na huduma za majifunzo, za kujiendelesha na za kutilia mkazo utafiti;
10. vyumba vya matibabu na vya huduma za jamii, kuajiri viongozi wa kazi za kiganga na za kilimo;
11. kuendesha mipango ya majira, ya kutafuta madini, kuchapa taswira na ya maji;
12. majanga ya kikawaida;
13. mitambo ya habari : redio, televisheni na viwanda vya sinema;
14. ukingo wa raia;
15. utalii;
16. haki za ardhi na madini, utengenezaji wa nchi, kawaida ya maji na misitu;
17. kutangulia magonjwa ya watu na ya minyama kwa faida ya raia;
18. ukingo wa mazingira, wa vituo vya asili na ulinzi wa vituo vya utalii;
19. kawaida kuhusu taratibu ya nguvu, ya mlimo, ya misitu, ya ufugo, ya bidhaa kutoka kwa minyama na kwa mimea;

20. kuunda shule za msingi na za sekondari, universiti na vyuo vikuu;
21. matembeleo ya baharini, nenda rudi za magari, kujenga na kutengeneza mabarabara ya kitaifa, kutoza na kugawa malipo ya matumizi ya mabarabara iliyojengwa na serikali kuu ao na jimbo;
22. vyumba vya matibabu na vya huduma za misaada;
23. fikara ya miswada, sera na mikataba ya mawasiliano ya kimataifa kuhusu utamaduni, sayansi na ujamii;
24. kuzaa, kuchukua na kutumia nguvu;
25. kinga ya makundi ya wazalili.

Kifungo cha 204*e*

Bila kuhasiri mipango mingine ya katiba hii, mambo yanayohusika na mamlaka pekee ya majimbo ni kama vile:

1. sera na mipango ya matengeneo ya jimbo;
2. mawasiliano kati ya majimbo;
3. watumishi wa serikali walioko jimboni na mitaani;
4. kutimiza kawaida kuhusu maisha ya raia;
5. mali ya jimbo;
6. madeni ya jimbo;
7. mikopo ya ndani kwa shida za jimbo;
8. kupana na kulinda hati za nyumba katika kuheshimu sharia ya kitaifa;
9. mipango ya biashara dogo dogo ya mipakani;

10. mipango ya uendeshaji wa idara za serikali, taasisi na mashirika ya serikali iliyoko jimboni kwa kuheshimu sharia ya kitaifa;
11. kuendesha kazi na mapatano ya kazi kwa faida ya jimbo na mitaa;
12. kununua vifaa kwa shida za jimbo;
13. shule za mwanzo, za msingi, za sekondari, za kazi na za kipekee, pamoja na kuelimisha raia kusoma na kuandika kwa mpango wa kawaida ya serikali kuu;
14. taratibu ya azabu na kutoza, za kifungo, kwa kuheshimu sharia na amri mbalimbali kuhusiana na sharia za kitaifa;
15. mawasiliano ya ndani ya jimbo;
16. kodi, ushuru na haki za jimbo na mitaa, yaani kodi ya udongo, kodi ya mapato ya kukodisha, kodi ya magari;
17. kubainisha mishahara ya jimbo kufwatana na sharia za kitaifa;
18. kuwapanga nafasi za kazi waganga kufwatana na kawaida ya watumishi wa idara za serikali, kutunga sera za usafishaji wa mazingira na kampeni za kupiganisha magonjwa kwa mujibu wa sera ya kitaifa : kupanga taasisi za afya na za kukinga magonjwa; kutumikisha na kuchungua utumikishaji wa kawaida za kitaifa kuhusu tiba na biashara ya madawa pamoja na kupanga taasisi za uganga wa kutibu, za huduma ya msaada na za kidini, majumba ya kutezama magonjwa, ya kupapasa na kuchungua madawa, mipango ya uimarishaji wa matibabu ya mwanzo;

19. kuandaa barnamiji ya madini, ya mawe ya samani, ya viwanda na ya nguvu za matumizi, kwa faida ya jimbo na kuitumikisha kufwatana na sera jumla ya taifa;
20. kuandaa barnamiji ya kilimo na misitu na kuitumikisha kwa kufwatia sera jumla ya taifa; kuwapanga nafasi za kazi watumishi wa idara za kilimo kwa kuheshimu kawaida msingi ya wafanya kazi wa serikali; kutumikisha mipango ya taifa kuhusu kilimo, misitu, mawindo, uvuvi, mazingira, ulinzi na nyika na ushikaji wa minyama ya pori; kupanga na kuchungua kampeni za ununuzi wa bizaa; kupanga bei ya bizaa;
21. kuwapanga kote jimboni waganga wa wanyama katika kuheshimu kawaida msingi ya wafanya kazi wa idara za serikali; kuandaa kampeni ya kutunza afya ya minyama na kuheshimisha hatua kuhusiana na afya ya minyama, hususa kuelekeana na vituo vya kupitia mipakani na hizo za utengaji;
22. kuendesha kampeni za kuwachanja minyama kwa kuzuwiya magonjwa; kuunda vituo vya utafiti na uchunguzi wa afya ya minyama, vituo vya utibabu wa minyama, pamoja na kuheshimisha sharia za taifa kuhusiana na afya ya minyama, mipangilio na ukuzaji wa afya ya msingi;
23. utalii, rasilimali ya kihistoria, mijumba ya umma na mashamba ya wanyama iliyoko jimboni;
24. makazi ya walioko mitaani na vijijini, mabarabara na vifaa vya jumla, vya jimbo na vya matarafa;
25. uchunguzi wa shuruli zote za kitamaduni na za michezo jimboni kote;

26. kuzitumikisha chemchem za kuzaa nguvu zisizokuwa za kinuklea, kutoa na kugawa maji kote jimboni;
27. kuzitumikisha hatua mbalimbali kuhusiana na haki ya makazi kwa wasiokuwa wakongomani, kufwatana na sharia za taifa;
28. kuzitumikisha desturi za kyenyeji;
29. kuandaa sera ya kuendesha jimbo.

Kifungo cha 205*o*

Bunge la jimbo haliwezi kutunga sharia kuhusu mambo yanayohusiana na mamlaka ya pekee ya serikali kuu. Vivo hivyo, chumba cha wateule ama seneti, haiwezi kutunga sharia kuhusu mambo yanayohusiana na mamlaka ya pekee ya jimbo.

Lakini, chumba cha wateule ama seneti, kinaweza, kwa njia ya sharia maalumu, kuipa Bunge ya jimbo uwezo wa kutunga sharia kuhusu mambo yanayohusiana na mamlaka pekee ya serikali kuu. Ikifikia wakati chumba cha wateule, ama seneti, kinaondoa uwezo kilichopeleka kwa Bunge la jimbo, sharia za jimbo zilizoiziniwa kuhusu mambo yanayohusu mamlaka pekee ya serikali kuu kwa mujibu wa uwezo huo, zinabaki kutumika ndani ya jimbo hadi pale itaiziniwa sharia ya taifa kwa kupanga taratibu kuhusu mambo hayo.

Vivo hivyo, Bunge la jimbo linaweza, kwa njia ya sharia, kukipa chumba cha wateule, ama seneti, uwezo wa kutunga sharia

kuhusu mambo yanayohusiana na mamlaka pekee ya jimbo. Ikifikia wakati Bunge la jimbo linaondoa uwezo uliopelekewa chumba cha wateule, ama seneti, sharia zilizoiziniwa kitaifa kwa mujibu wa uwezo huo, zinabaki kutumika ndani ya jimbo hadi pale itaiziniwa sharia ya jimbo kwa kupanga taratibu kuhusu mambo yale.

Ama kuhusu mambo yanayohusiana na mamlaka ya kuchangia kati ya serikali kuu na jimbo, sharia yoyote ya jimbo ambayo inaenda kinyume na sharia ama kawaida ya utendeji ya kitaifa, inabatilika yenyewe.

Sharia za kitaifa zina uwezo juu ya sharia za jimbo.

Kifungo cha 206*a*

Isipokuwa tu kwa mipango mingine tofauti ya sharia za kitaifa, serikali za majimbo zinatumikisha, kwa niaba ya idara zao mbalimbali, sharia na kawaida za taifa.

Kifungo cha 207*a*

Unajulikana utawalo wa asili.

Unapewa kwa mujibu wa desturi ya kyenyeji, kama desturi hiyo haiende kinyume na katiba, na sharia, na mipango ya ukimya na mila mizuri.

Sultani wa asili yeyote anayehitaji kupata wazifa wa kuchaguliwa, analazimika kupita kwa machaguzi, ila tu kama

akifanikiwa na maagizo ya sehemu ya tatu ya kifungo cha 198 cha katiba hii.

Mtawala wa asili analazimishwa kukuza muungano na mfungamano wa taifa.

Sharia maalumu inabainisha kawaida ya masultani wa asili.

MLANGO WA TANO
KUHUSU HALMASHAURI YA
KIUCHUMI NA YA KIJAMII

Kifungo cha 208*e*

Inaundwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo Halmashauri ya kiuchumi na kijamii.

Kifungo cha 209*a*

Halmashauri ya kiuchumi na kijamii inahusika na kutoa maoni na fikara kuhusu maswali ya kiuchumi na kijamii iliyopelekewa na Rais wa Jamhuri, na Chumba cha wateule, na seneti ao na serikali.

Inaweza, kwa fikara yake pekee, kuizinduwa serikali kuu na majimbo kuhusu mabadiliko muhimu inayozanika kuweza kurahisisha maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii nchini.

Kifungo cha 210*i*

Sharia maalumu inabainisha mpango na uendeshaji wa halmashauri ya kiuchumi na kijamii.

## MLANGO WA SITA
## VYUMBA VYA KULINGANIA DEMOKRASIA

### KIPINDI CHA KWANZA
### KUHUSU TUME HURU YA TAIFA
### IHUSIKAYO NA UCHAGUZI

Kifungo cha 211*a*

Inaundwa Tume Huru ya taifa inayohusika na uchaguzi, ikiwa na nafsi yake mbele ya sharia.

Tume hii inahusishwa na kuendesha mipango yote ya machaguzi, kama vile kuandikisha wapiga kura, kutunga daftari za machaguzi, kusimamia kura, kuhisabu kura, na matokeo yote yanayohusiana na kura ya maoni.

Inapewa uzito wa ukawaida wa mipango ya uchaguzi na kura ya maoni.
Sharia maalumu inabainisha mipango na uendeshaji wa Tume huru ya taifa ihusikayo na uchaguzi.

## KIPINDI CHA PILI
## KUHUSU HALMASHAURI KUU YA MITAMBO YA HABARI NA MAWASILIANO

Kifungo cha 212*i*

Inaundwa halmashauri kuu ya mitambo ya habari na mawasiliano ikiwa na nafsi yake mbele ya sharia.

Halmashauri inahusika na kulingania uhuru na kinga ya mitambo ya habari na njia zote za mawasiliano kati ya watu, katika kuheshimu maagizo ya sharia.

Inachungulia pia heshima ya kanuni za kazi ya kupasha habari na kutekeleza usawa wa matumizi ya vyombo vya habari vya serikali kwa faida ya vyama vya siasa, mashirika na wananchi.

Utungo, mamlaka, mipangilio na uendeshaji wa halmashauri vinabainishwa na sharia maalumu.

## MLANGO WA SABA

# KUHUSU MIKATABA NA MAKUBALIANO YA KIMATAIFA

## Kifungo cha 213*u*

Rais wa Jamhuri ndie anashurulikia na kuratibisha mikataba na makubaliano ya kimataifa.

Serikali inafanya mapatano na mataifa mengine ambayo haihusike na kuratibishwa na Rais, inajadili kwenyi baraza la mawaziri na kuvijulisha vyumba vya bunge.

## Kifungo cha 214*e*

Haiwezi kuratibishwa na Rais, ila kwa mujibu wa sharia maalumu, mikataba ya amani, mikataba ya biashara, mikataba na makubaliano kuhusu mashirika ya kimataifa, mikataba ao mapatano inayohusisha mali ya serikali, inayobadilisha maagizo ya sharia, inayohusu hali ya watu, inayohusu kubadilishana ardhi ao kuunganisha maeneo ya ardhi.

Haina samani makubaliano yoyote ya kukata, kubadilisha ao kuunga sehemu ya ardhi bila izini ya raia wakongomani kwa kupitia njia ya kura ya maoni.

## Kifungo cha 215*o*

Mikataba na makubaliano ya kimataifa inayoratibishwa inao uwezo zaidi ya sharia, pale tu inapotangazwa, kwa sharti kwa kila mkataba utekelezwe na upande mwengine.

Kifungo cha 216*a*

Ikiwa kama Korti Kuu ya Katiba, kwa maombi ya Rais wa Jamhuri, ya serikali ao ya kikumi kimoja cha wateule wa taifa ao wa seneti, itaamua kwamba mkataba fulani una ndani mwake kifungo kisichoafikiana na katiba ya Jamhuri, hautaratibishwa mkataba huo ila baada ya kurekebisha katiba.

Kifungo cha 217*a*

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inaweza kusaini mikataba na makubaliano ya ushirika ao ya ujumuiya kwa nia ya kukuza umoja wa kiafrika, hata ikiwa kama mikataba hiyo italazimu kuachilia kiasi fulani cha enzi ya taifa.

## MLANGO WA NANE
## KUHUSU MAREKEBISHO YA KATIBA

Kifungo cha 218*e*

Fikara ya kurekebisha katiba inawahusu, kwa kila yule :

1. Rais wa Jamhuri;
2. Serikali, baada ya mjadala wa baraza la mawaziri;

3. kila chumba cha bunge kwa maombi ya nusu kati ya memba wake;
4. baadhi ya raia wakongomani, kwa idadi ya watu laki moja (100.000) wakipeleka maombi yao mbele ya chumba kimoja cha bunge.

Kila fikara inapelekwa mbele ya chumba cha wateule na mbele ya seneti ambao, kila chumba, watachukua hatua inayofaa kwa sauti ya uwingi wa kawaida, yaani zaidi ya nusu kati, baada ya kutizama umuhimu wa fikara ao maombi ya marekebisho.

Marekebisho yenyewe hayana nguvu ila pale pendekezo, muswada ao maombi, itakubaliwa na kura ya maoni.

Lakini, haitalazimishwa pendekezo, muswada ao maombi kupigiwa kura ya maoni ikiwa kama chumba cha wateule na seneti vitajumuika katika kongresi na kuikubali madai ya marekebisho kwa kura ya asili mia sitini (60%) ya jumla ya memba wa kongresi.

Kifungo cha 219*a*

Haiwezi kufanyika marekebisho yoyote ya katiba wakati wa vita, wakati inatangazwa hali ya wasiwasi ao ya zarura, wakati anaongoza nchi Rais wa mda, ao wakati chumba cha wateule na seneti vimo katika kizuwizi cha kukutana.

Kifungo cha 220*i*

Umbo la kijamhuri inayopewa nchi, mfumo wa kura ya raia, hali ya serikali ya uwakilishi kamili, idadi na mda wa mihula ya Rais wa Jamhuri, uhuru wa korti na mahakama, mfumo wa uwingi wa vyama na mashirika ya utetezi wa wafanya kazi, haviwezi kamwe kubadilishwa.

Ama tena, inaharamishwa kabisa marekebisho yoyote ya katiba ambayo shabaha yake ni kupunguza haki na huru za mwanaadamu, ao kupunguza mamlaka ya majimbo na maeneo ya kujimiliki.

## MLANGO WA TISA
## KUHUSU MIPANGO YA MPITO
## NA YA MWISHO

Kifungo cha 221*a*

Sharia na kawaida zote zinazoendesha nchi leo, ikiwa kama haziende kinyume na katiba hii, zinaendelea kutumika hadi zitapobatilishwa na kubadilishwa.

Kifungo cha 222*i*

Vyumba vya uongozi wa taifa vya serikali ya mpito, vinaendelea na kazi zake, kufwatana na katiba ya mpito, hadi vitapotawazishwa vyumba vingine vinavyopangwa na katiba hii.

Vyumba vya kulingania demokrasia vinavunjika vyenyewe hapo tu itatawazishwa bunge mpya.

Bali Bunge inaweza, ikilazimika, kuunda vyumba vingine vya kulingania demokrasia, kwa sharia maalumu.

Kifungo cha 223*u*

Kabla iwekwe Korti Kuu ya Katiba, Halmashauri ya Serikali na Mahakama Kuu, Mahakama Kuu iliyoko leo inaendesha shuruli zinazovihusu kwa mujibu wa katiba hii.

Kifungo cha 224*e*

Kabla viwekwe vyumba vya sharia vya uongozi, korti kuu za majimbo ndio zinahusika na kuendesha mamlaka inayopangwa kuhusu korti kuu za uongozi majimboni.

Kifungo cha 225*o*

Korti ya usalama wa nchi inavunjika yenyewe pale tu itaanza kutumika katiba hii.

Kifungo cha 226*a*

Maagizo ya sehemu ya kwanza ya kifungo cha pili cha katiba hii itaanza kutumika kwa kipindi cha miezi salasini na sita (36) kitachofwatia kutawazishwa vyumba vya utawalo vinavyopangwa na katiba hii.

Kabla ya hapo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo itabaki na mji wa Kinshasa na majimbo kumi, ikiwa kila ile na nafsi yake mbele ya sharia. Nayo ikiwa ni, (1)Bandundu, (2)Ekwatori, (3)Jimbo la mashariki, (4) Kasai ya magharibi, (5)Kasai ya mashariki, (6)Katanga, (7)Kivu ya Kaskazini, (8)Kivu ya kusini, (9) Kongo ya chini na (10) Maniema.

Kifungo cha 227*a*

Kama inavotajwa kunako kifungo cha pili cha katiba hii, majimbo hayo (25) ndio vitongoji vya uchaguzi wa wanaseneti kwa awamu hii ya kwanza.

Sharia itabainisha jinsi ya kuupa mji wa Kinshasa idadi nyingine ya juu kwa uchaguzi wa wanaseneti.

Kifungo cha 228*e*

Bila kuhasiri sehemu ya kwanza ya kifungo cha 222, katiba ya mpito ya tarehe 4 aprili 2003 inabatilika yote nzima.

<u>Kifungo cha 229*a*</u>

Katiba hii inayokubaliwa kwa kura ya maoni ya raia wakongomani, inaanza kutumika tangu kuiziniwa kwake na Rais wa Jamhuri,

Pa Kinshasa, tarehe ....../...../200...

Joseph KABILA,

## ANGALISHO

Kwa maombi ya wasahihishaji wa tafsiri hii ya kiswahili, imetumiwa maneno ya lugha kufwatana na maandishi yake ya kawaida ya kiswahili sanifu.

Tutakuombeni, enyi wasomaji watukufu, kila mtapokutana na maneno hayo, basi, kumbukeni angalisho hii.

Mchanganiko wa herufi D na herufi H, yaani DH, hutamkwa kwa kiswahili Z ulimi ukigusa meno ya juu.
Mfano ARDHI hutamkwa ARZZI
MADHUMUNI hutamkwa MAZZUMUNI

Mchanganiko wa herufi G na herufi H, yaani GH, hutamkwa HR ikitokea kwenyi koo pamoja na kusukuma pumzi.
Mfano BUGHUZA hutamkwa BUHRUZA
GHARAMA hutamkwa HRARAMA

BALEGHE hutamkwa BALEHRE

Mchanganiko wa Herufi T na herufi H, yaani TH, hutamkwa S pamoja na ulimi ukigusa meno ya juu.
Mfano THABITI, hutamkwa SSABITI
THALASINI hutamkwa SSALASINI,

Na vvhv.

Tunapeleka shukrani zetu za tele kwa kikundi cha wasahihishaji wa lugha ya Kiswahili wa jimbo la Maniema, waliochunguza kwa makini kabisa na kukubalisha tafsiri inayotangazwa hapa leo, nao ni akina Bwana na akina Bibi

1. SHABANI MWANAOMBA
2. MUTHOMA BUSHIRI
3. GERTRUDE SUMAILI
4. MUTINGWA DAULA MUNDAMA
5. SHINDANO KOKO WA MWENDA
6. DJUMA ASSANI KAPITENI
7. MIANZI BWA SAIDI
8. SADIKI ABEDI MGENI
9. AWAZI TATA RAMAZANI

KIJITABU HICHI KINACHAPISHWA
KWA MSAADA WA KITAALAMU
NA WA MALI KUTOKA KWA
E I S A/RDC